

**Lulu** Diva agunaguna kujichubua

UKURASA 20



**Kane** hatihati kucheza fainali

UKURASA 21

## MAISHA

Nipashe Baba, Mama na Mwana *Jumapili*



Analilia simu janja, nani alimfundisha?



MAISHA NI NYUMBA
Zulia ndani ya nyumba ni muhimu



HARUSI



ZIJALI NYWELE ZAKO
Kitunguu maji, tangawizi suluhisho tosha

UKURASA 9


# Nipashe JUMAPILI

Jumapili Aprili 25, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0580561

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Siri zaidi hasara ATCL zafichuka




UKURASA 2

## YALIYOMO


UKURASA WA 3
**KASI KIMBUNGA JOBO YAPUNGUA, MVUA KUBWA YAJA**
MAMLAKA ya Hali ya Hewa (TMA) imesema kasi ya kimbunga Jobo...

UKURASA WA 4
**CHADEMA KUMFIKISHA SPIKA KORTINI**
BAWACHA wanakusudia kufungua shauri mahakamani dhidi ya Spika Job Ndugai...

UKURASA WA 5
**AUAWA NA WANAFUNZI TUHUMA KUIBA GODORO**
WATU wawili wakazi wa Wilaya za Lindi na Ruangwa mkoani...


## Wizi vifaa vya magari, pikipiki ulivyorejea kwa kasi nchini

UKURASA 2







Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Abubakar Kunenge, akiangalia moja ya vifaa vya magari jana, vilivyokamatwa na Jeshi la Polisi mkoani humo, katika operesheni ya kukamata wahalifu vinara wanaojihusisha na wizi wa pikipiki, magari na vifaa/vipuri vya magari. Watuhumiwa 49 wametiwa mbaroni. Kushoto kwake ni Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa. **NA MPIGAPICHA WETU**



# Lissu aibua mambo hotuba ya Samia

UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


**MICHEZO** YANGA, AZAM FC HESHIMA, KISASI UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

## Wizi vifaa magari, pikipiki ulivyorejea kwa kasi nchini

**Na Romana Mallya**

WIZI wa vifaa vya magari na pikipiki umeripotiwa kurejea kwa kasi maeneo mbalimbali ya nchi, hususan mkoani Dar es Salaam, huku Jeshi la Polisi likibainisha namna wahalifu wanavyoiba, kutenganisha na kwenda kuviuza vifaa kwa madai kuwa vimeagizwa kutoka nje.

Katika operesheni yake dhidi ya wahalifu hao, Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, hadi kufikia jana jioni, lilikuwa linawashikilia watuhumiwa 49 pamoja na vifaa mbalimbali vinavyosadikiwa kuwa vya wizi.

Lazaro Mambosasa, Kamanda wa Polisi wa Kanda hiyo, aliiambia Nipashe jana jioni kuwa wamebaini kuwa baada ya wahalifu hao kuiba vifaa kwenye magari au pikipiki, wanatenganisha na vifaa hivyo wanaviuza kama wameviagiza kutoka nje ya nchi.

"Wanaviingiza kwenye yadi, wanayachinja (kutenganisha) halafu vifaa vya magari vinarudi kama vifaa vilivyotumika (used) na hii inatokana na zuio la usafirishaji lililotokana na janga la corona ambalo limesababisha tatizo hili," alisema.

Kamanda Mambosasa alisema operesheni ya ukamataji wa wahalifu vinara wanaojihusisha na wizi wa pikipiki, magari na vifaa au vipuri vya magari pamoja na wauzaji na wanunuzi wa vifaa hivyo inaendelea.

"Jumla ya watuhumiwa 49 wamekamatwa katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Dar es Salaam wakiwa na pikipiki 10 za aina mbalimbali na vifaa vyake, gari moja aina Toyota Noah likiwa limetolewa viti ambalo limekuwa likitumiwa na wahalifu kubebea mali za wizi," alibainisha.

Kamanda Mambosasa alisema watuhumiwa hao walikamatwa na vifaa vya aina mbalimbali vya magari kama vile milango, vioo vinavyoongoza madereva (side mirrors), power windows, redio za magari, bodi za mbele za magari ya aina mbalimbali na taa.

"Majina ya watuhumiwa kwa sasa yanahifadhiwa kwa sababu za kiupelelezi na operesheni. Hii ya ukamataji bado inaendelea," alisema.

Kiongozi huyo wa polisi alisema watuhumiwa wote wanaendelea kuhojiwa na watafikishwa mahakamani baada ya kukamilisha taratibu zote za kisheria.

Alitoa wito kwa jamii kuendelea kutoa ushirikiano kwa kutoa taarifa za uhalifu na wahalifu ili kuendelea kuimarisha usalama katika mkoa huo wa kibiashara.

"Tunatoa onyo kwa watu wote wanahojihusisha na wizi wa magari, pikipiki na vifaa au vipuri vya magari kuacha mara moja kwani tumejipanga na tutawafikia popote watakapokimbilia au kujificha," alisema.



Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Brigedia Jenerali John Mbungo, akirejesha fedha zaidi ya Sh. Bilioni 1.36 kwa wawakilishi wa taasisi za umma, mfuko wa pembejeo wa Taifa, vyama vya kuweka na kukopa (SACCOS) vya mkoani Arusha, mifuko ya jamii ikiwemo PSSSF, NSSF na baadhi ya wananchi waliotapeliwa fedha zao, jijini Arusha jana, zilizookolewa na taasisi hiyo, baada ya kuchepushwa kwa njia ya rushwa na ubadhirifu. **PICHA: ALLAN ISACK**

# Siri hasara ATCL sasa hadharani

**Na Enock Charles**

SHIRIKA la Ndege Tanzania (ATCL), limebainisha kuwapo masharti magumu katika mkataba wa ukodishaji ndege kati yake na Wakala wa Ndege za Serikali (TGFA).

Limesema masharti hayo yanayohusisha lilichokiita tozo zisizoendana na uhalisia, ni miongoni mwa sababu za shirika hilo kujiendesha kwa hasara ya mabilioni ya shilingi.

Hayo yalibainishwa jana jijini Dar es Salaam na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa shirika hilo, Albinus Manumbu, wakati wa mkutano wa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara na taasisi zilizo chini ya wizara hiyo.

"Mheshimiwa Naibu Waziri, hizi ndege ambazo ATCL inaziendesha ni mali ya serikali na anayezimiliki ni TGFA, shirika linawajibika kulipa kodi. Mojawapo ya gharama za uendeshaji ambazo ATCL inaingia ni zile kodi inazotozwa.

"Katika umiliki huwa kuna mkataba na ule mkataba kwa sasa siyo rafiki kwa sababu kuna viwango vikubwa vya tozo kuliko uhalisia, lakini pia ule mkataba TGFA hana uwezo wa kusimamia.

"Kwa mfano, kuanzia mwezi wa tatu (Machi) mpaka mwezi wa sita (Juni) tulipopita kwenye corona, bado tuliendelea kuchajiwa. Kwa hiyo tulichajiwa kodi ya ukodishaji ambayo hatujazalisha," alisema.

Aliitaja sababu nyingine ya kutokea kwa hasara ya kiuendeshaji katika shirika hilo kuwa ni kurithiwa kwa madeni ya shirika tangu kuanzishwa kwake.

Alibainisha kuwa madeni hayo yamezalisha riba ya kiasi cha Sh. bilioni 16 na matengo (provision) inayotokana na kesi mbalimbali pamoja na madeni ambayo shirika linadai sehemu mbalimbali.

Manumbu alitoa ufafanuzi huo baada ya Waitara kumtaka aeleze kwa kina sababu za kuwapo kwa hasara ya kiuendeshaji kwa shirika. Baada ya ufafanuzi huo, Waitara alilitaka shirika hilo kurekebisha kasoro zilizopo ili lijiendeshe kwa faida ikiwamo kuimarisha usimamizi na mazingira ya kazi kwa wafanyakazi wake huku akiahidi serikali kufanya maboresho kadhaa ndani ya shirika hilo.

"Mheshimiwa Rais ameshatoa maelekezo mahususi kwamba ataangalia na kuondoa changamoto zinazolikabili shirika, lakini kuondoa changamoto ni jambo moja, tunachotaka ni kwamba taasisi isimamiwe vizuri ikiwamo kuboresha mazingira ya kazi, mapato na matumizi, huduma kwa wateja zivutie, kwa sababu soko la dunia ni ushindani.

"Mtu atakayekuwa na lugha nzuri ya mapokezi kwa wateja wake ndiye atakayepata soko. Kwa hiyo lazima ATCL ijiandae kiushindani zaidi wakati serikali inachukua hatua kutekeleza maelekezo ya Rais kuondoa changamoto zinazowakabili," aliagiza.

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha 2019/20, iliyowasilishwa bungeni wiki mbili zilizopita, inabainisha kwamba ATCL imetengeneza hasara ya mabilioni kwa miaka mitano mfululizo. Katika ripoti yake hiyo, CAG Charles Kichere, anabainisha kuwa hadi kufikia Juni 30, mwaka jana, serikali ilikuwa imenunua ndege nane kwa gharama ya Sh. trilioni 1.028 katika juhudi za kufufua ATCL.

"Ndege hizo zinamilikiwa na Wakala wa Ndege za Serikali na ATCL huzikodisha. Pamoja na kununua ndege, kwa miaka mitano, yaani kuanzia 2015/16 hadi 2019/20, serikali imeisaidia ATCL kiasi cha Sh. bilioni 153.711 kwa ajili ya shughuli za uendeshaji na maendeleo.

"ATCL imekuwa ikitengeneza hasara kwa miaka mitano mfululizo na mwaka huu wa ukaguzi (2019/20) ilitengeneza hasara ya Sh. bilioni 60.246. Kwa miaka mitano, imetengeneza hasara ya Sh. bilioni 153.542," CAG anabainisha kwenye ripoti yake hiyo.

Katika mkutano wake wa jana, mbali na maelekezo kwa ATCL, Waitara pia aliitaka Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu (LATRA) kutatua kero zilizopo kwenye mfumo wa kukata tiketi kwa njia ya mtandao, ili kuondoa malalamiko yaliyopo.

Mbali na ATCL na LATRA, taasisi zingine zilizokuwa na uwakilishi katika mkutano huo wa Waitara, ni pamoja na Chuo cha Usafirishaji cha Taifa (NIT), TAZARA, Wakala wa Barabara (TANROADS), Kampuni ya Meli ya Tanzania na China (SNOTASHIP), Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA), Mamlaka ya Bandari (TPA) na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA).

# Mbaroni tuhuma ya kuwa na shamba la bangi

**Na Gurian Adolf, RUKWA**

JESHI la Polisi mkoani Rukwa, limewakamata watu 30 katika operesheni maalum, wakituhumiwa kwa makosa mbalimbali likiwamo la kumiliki shamba la bangi.

Taarifa iliyotolewa jana na Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani humo, Theopister Mallya, ilibainisha kuwa watuhumiwa hao wanadaiwa kufanya makosa ya kuvunja na kuiba, wizi wa pikipiki na kumiliki shamba lenye ukubwa wa ekari moja na nusu wakiwa wamelima bangi.

Alisema operesheni hiyo ilifanyika katika maeneo tofauti ya mkoa huo, akibainisha kuwa katika tukio la kwanza, watu 15 wanaodaiwa kujihusisha na vitendo vya kuvunja nyumba za watu na kuiba, walikamatwa wakiwa na mali za wizi na vifaa wanavyotumia wakati wa kuvunja.

Kamanda Mallya alisema kuwa katika tukio la pili, watu watatu walikamatwa na pikipiki tano zinazodaiwa za wizi.

Alisema katika tukio la tatu, watu 12 walikamatwa wakidaiwa kumiliki shamba la bangi ekari 1.5 pamoja na bangi kavu yenye uzito wa Kg 25 wakiwa wamezihifadhi ndani.

Alidai kuwa watu hao wamekuwa wakiuza dawa hizo za kulevya katika maeneo mbalimbali ndani na nje ya Mkoa wa Rukwa.

Alisema watuhumiwa wote hao wanashikiliwa na watafikishwa mahakamani mara baada ya upelelezi kukamilika.

# Matatani kuchelewesha vibali vya uwekezaji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, ametoa siku tano kupewa taarifa ya sababu ya kuchelewa kutolewa kwa vibali tisa vya wawekezaji ambavyo maombi yao yaliwasilishwa tangu mwaka jana.

Vilevile, ameagiza kufanyika kwa mapitio ya sheria na Sera ya Uwekezaji ili kuona kama kuna haja ya kufanya maboresho kutokana na vikwazo vilivyopo na taarifa hiyo iwasilishwe mezani kwake Mei 15, mwaka huu.

Akizungumza na wafanyakazi wa Idara ya Kazi katika wizara hiyo jana, Waziri Mhagama alisema ucheleweshaji huo unaweza kutafsiriwa kuwa ni harufu ya rushwa, hivyo ofisi yake haitavumulia suala hilo.

"Ninajua vipo vibali tisa vimelalia tangu mwaka jana, ningependa kujua vibali hivyo tangu mwaka jana kwanini havijafika kwako Kamishna wa Kazi na pia ninataka nijue waliochelewesha, siwezi kuwavumilia vibali hivi ni vingi, hadi kufika Jumatano nijue aliyekuwa navyo alikuwa na makusudi gani, na amechukuliwa hatua gani," alisema.

Alisema hatakuwa na msamaha kwa watakaobainika kuchelewesha kwa makusudi.

Akizungumzia kuhusu maboresho ya sera na sheria, alisema endapo kuna haja ya kufanya hivyo, watashirikiana na Bunge ili kufanya mabadiliko ikiwa ni pamoja na kuangalia tozo na ada mbalimbali zilizowekwa.

"Kumekuwa na mgongano wa sheria kati ya taasisi moja na nyingine, tumekuwa na mgongano labda wa kisera kutoka taasisi moja na nyingine. Mei 15 maeneo hayo yote yafanyiwe kazi, yawe mezani kwangu. Kama ni kanuni, nitabadili haraka lakini ikiwa ni sheria tutamwomba Rais kibali cha dharura ili tupeleke bungeni na kubadili haraka," alisema.

Mhagama alisema lengo ni kuweka vigezo ambavyo vitaleta motisha kwa wawekezaji.

Awali, Naibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Kazi (Ajira, Kazi na Vijana), Patrobas Katambi, alibainisha matatizo yanayosababisha kuchelewa na kukosekana kwa vibali na kuwataka vishoka na madalali kuacha mara moja.

# Lissu aichambua hotuba ya Samia

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, ameichambua hotuba ya wiki hii ya Rais Samia Suluhu Hassan na kutaja alichotamani kisemwe na Mkuu wa Nchi huyo lakini amekikosa.

Lissu, akiizungumzia hotuba hiyo jana, alisema kuwa kwa kiasi kikubwa ilikuwa ni marudio ya hotuba aliyowasilisha bungeni Novemba mwaka jana na mtangulizi wake, Hayati Dk. John Magufuli.

Alisema wanachohitaji sasa kutoka kwa Rais Samia ni kile alichokiita ramani ya kurudisha demokrasia na haki nchini.

"Tunachohitaji ni mazungumzo yetu, utekelezaji, kuna mambo ambayo hayahitaji mazungumzo na sisi, kwa miaka mitano tumekatazwa kufanya mikutano ya siasa bila msingi wowote wa kisheria. Rais Samia kusema hayo makatazo hayatakuwapo tena, haihitaji kubadilisha sheria bali kutoa kauli," alisema.

Lissu alisema alitamani kusikia kwenye hotuba ya Rais Samia likizungumziwa suala la kesi alizodai za kubambikwa dhidi ya baadhi ya wananchi na kupiga marufuku kukamatwa kwa watu na kufunguliwa kesi za aina hiyo.

"Tumeteswa, tumepigwa, wengine tumeponea chupuchupu, tumekimbilia uhamishoni, haihitaji nusu saa kusema kwamba haya mambo kwenye serikali yangu ni marufuku.

Hawa waliokimbia nchi kwa kuogopa maisha yao, warudi nyumbani watakuwa salama, hii haihitaji nusu saa," alisema.

Lissu alisema kauli kama hizo ambazo hazihitaji mabadiliko ya kisheria, zingetengeneza mazingira mazuri ya mazungumzo anayokusudia kufanya Rais Samia na vyama vya siasa.

"Ili tuzungumze kwenye haya mengine ambayo yanahitaji mabadiliko ya katiba, sheria na kitaasisi, Nelson Mandela na wenzake walikuwa magereza ya makaburu miaka saba, walipotaka mazungumzo cha kwanza walifungulia wafungwa wa kisiasa, wakafungulia maelfu waliokuwa magereza ya makaburu.

"Tunataka mazingira ya namna hii, haihitaji mabadiliko ya kisheria. Binafsi nilitazamia fursa ya mama (Rais Samia) kuzungumza na taifa, angezungumza kubwa la namna ya kuponya haya maumivu," alisema.

Lissu pia alibainisha kuwa juzi CHADEMA ilipokea barua ikiitaka iwasilishe kwa Mwenyekiti wa Baraza la Vyama vya Siasa, John Shibuda, ajenda zao ambazo wanataka kuzungumza na Rais Samia.

"Yaani CHADEMA tupeleke mambo tunayotaka kuzungumza na Rais, tupeleke kwa Shibuda? Au kwa Msajili wa Vyama vya Siasa? Yaani Msajili atutengenezee ajenda za kuzungumza na Rais?

"Sisi siyo watoto wadogo, hatuwezi kutaka kuzungumza na Rais halafu tupeleke kwa Msajili. Msajili kazi yake ni kushughulikia usajili wa vyama, siyo kuwa msemaji wetu," alisema.

Lissu alisema wanataka kila chama kiende na ajenda yake na kama Rais anataka kuandikiwa ambayo wanataka kuzungumza naye, watamwandikia.

Alisema walipoandika barua kwa Rais hawakusahau kama kuna Baraza la Vyama vya Siasa ambapo Shibuda ni mwenyekiti wake na kufafanua kuwa wakiwataka kuwasiliana naye, sheria haisemi mpaka wapitie kwenye baraza hilo au kwa Msajili.

Alisema hana taarifa kama kuna chama kingine chochote kimeomba kukutana na Rais.

"Tunahitaji kuzungumza ajenda ya demokrasia, mabadiliko ya katiba na sheria, ajenda itakayobadili Tume ya Taifa ya Uchaguzi ili tupate uchaguzi huru na haki zitakazowapatia wabunge wa maana na siyo vivuli," alisema.

# Kasi kimbunga Jobo yapungua, mvua kubwa yaja

**Na Romana Mallya**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa (TMA) imesema kasi ya kimbunga Jobo imepungua, huku ikitahadharisha uwezekano wa kunyesha mvua kubwa inayofikia milimita 200 hadi 400 kwa saa 24 kuanzia jana usiku.

Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dk. Agnes Kijazi, akizungumza jana na Televisheni ya Taifa (TBC), alisema kutokana na kuwapo kwa mkandamizo mdogo wa hewa, wanatarajia mvua itaongezeka kadri kimbuka kinapokuja ukanda huo.

Alisema athari zilizotarajiwa ni pamoja na upepo mkali, lakini kasi ya kimbunga hicho imepungua na hivyo mvua kubwa zinatarajiwa kunyesha katika mikoa ya Dar es Salaam na Mtwara.

"Kadri nikavyoendelea kusogea, tunatarajia kutakuwa na ongezeko la mvua na sasa hivi tayari katika eneo la Mkoa wa Lindi na Kisiwa cha Mafia kuna mawingu mazito na mvua imeanza kunyesha kidogo kidogo, hadi jioni (jana) tunategemea mvua kuongezeka katika Kisiwa cha Mafia na Mkoa wa Lindi," alisema. Dk. Kijazi alisema Mkoa wa Dar es Salaam ulitarajiwa kuanzia jana usiku kupata mvua kubwa kutokana na mkandamizo hafifu uliotarajiwa kuwa umesogea na kufika maeneo hayo.

"Maeneo ya Mtwara mawingu yanasogea hivyo nayo usiku wa leo (jana) yatapata mvua kubwa, kuanzia usiku hadi kufikia kesho yaani ndani ya saa 24, maeneo haya yatapata mvua kubwa ambayo ni milimita 200 mpaka 400," alisema. Alisema kiwango hicho cha mvua ni kikubwa zaidi ya mvua ambayo inanyesha katika mwezi mzima wa Aprili.

Dk. Kijazi alisema ukipata mvua kubwa namna hiyo kwa siku moja ambayo ingeweza kutawanyika na kunyesha mwezi mzima inaweza athari za mafuriko zinaweza kujitokeza.

"Ni vizuri wananchi wa mabondeni wakachukua tahadhari na watumiaji wa bahari, wavuvi wanaokwenda baharini alfajiri, uwezo wa kuona mbali utapungua na uzito wa boti zao, wanaosafiri kwa bahari waendelee kuzitumia taarifa," alisema.

Pia alisema Jumatatu na Jumanne kutakuwa na hali ya mvua na mamlaka itaendelea kufuatilia viwango vyake.

Wakati TMA ikitoa tahadhari hiyo, Mufti Mkuu wa Tanzania, Sheikh Abubakar Zuberi, amewataka masheikh wa mikoa, wilaya, kata, maimam na viongozi wa dini kufanya dua maalum kwa ajili ya kumwomba Mungu anusuru taifa dhidi ya janga hilo la kimbunga cha Jobo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mkoani humo, Sheikh Zuberi aliwataka wafanye hivyo kila baada ya swala kuliombea taifa pamoja na majanga mengine. "Kila muumini afanye dua na sala usiku wa kuamkia kesho (leo), binafsi nitaongoza dua maalum kupitia kipindi cha Ramadhani Kareem leo (jana), ninawaalika waislam wote tushirikiane katika dua hii," alisema


**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya**
**Kituo Cha KINGOLWIRA**
**Usimamizi wa mirathi Na 10/2021**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU SHABANI KISANYWA WA KINGO MOROGORO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA ALLY SHABANI KISANYWA**

**TANGAZO**

(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu. Wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 19mwezi 05 Mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo
Zingatia
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa
*Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani na waweza kukaguliwa
*Marehemu hakuacha wosia
* Futa isiyohusika

**Imetolewa leo Tarehe 19 mwezi 4 Mwaka 2021**



**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi**
**NO.101/2021**

**Ombi la HADIJA ALLY NG'ADOA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu CODSON LAMECK MSEMWA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 13/05/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo . Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.
Tarehe 13/04/2021



bgtl

**BEST GROUP (T) LIMITED**
Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa idhini tuliyopewa na **BANK OF AFRICA (BOA)** Tutauza kwa mnada wa hadhara dhamana ya mkopo wa mdaiwa wao ambayo ni nyumba iliyopo msasani peninsula. ili Kufika kwenye nyumba unapitia mtaa wa sandvik ambayo inapakana na chole road karibu kabisa na Transit supermarket kituo cha basi. Alama muhimu ni jengo la NHC, Valhalla Estate na Old Nasaco flats. Iwapo mdaiwa hatalipa deni lake lote ndani ya siku ishirini na moja (21) kuanzia tarehe ya tangazo hili, dhamana ya mkopo wake itauzwa kwa njia ya mnada wa hadhara.

| JINA LA MDAIWA /MDHAMINI | MAELEZO YA DHAMANA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|
| WANTANSHI LOUNGE | Nyumba ya makazi yenye Hati Na. 23659, Kiwanja Na.1318, Ofisi ya ardhi Na. 398447, Iliyopo Msasani Peninsular, Dar Es Salaam. Kwa jina la **Cecylia Mtwale Chinn** | 21 .05.2021 |

**MASHART YA MNADA**
1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hiyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa taarifa zaidi wasiliana na:**
**Mkurugenzi Mtendaji**
**Best Group (T) Ltd**
**Alli Hassan Mwinyi Road.**
**Green Acres Buliding, 2nd Floor.**
**P.O. Box 1088**
**Dar Es Salaam**
**Mobile + 255 715-363537/766-309913**

**Au**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**Bank of Africa Plc**
**P. O. Box 3054 Dar Es Salaam**

## CHADEMA kumfikisha Spika kortini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BARAZA la Wanawake wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAWACHA), linakusudia kufungua shauri mahakamani kama kile linachokiita katiba ya nchi kuendelea kukiukwa kwa Spika wa Bunge, Job Ndugai, kuruhusu wabunge 19 wanaotokana na chama hicho kushiriki vikao vya Bunge licha ya kuvuliwa uanachama.

Mwekahazina wa BAWACHA Taifa, Catheren Ruge, aliyasema hayo jana jijini Dodoma alipozungumza na waandishi wa habari na kutoa tamko la baraza hilo juu ya suala hilo.

Ruge alisema baraza hilo halitakaa kimya pale linapoona katiba ya nchi inavunjwa na watu kwa makusudi.

"Hatutakaa kimya mpaka haki ipatikane, katiba ya nchi lazima tuilinde kwani wabunge hawa ambao wapo bungeni hawana sifa kwa mujibu wa katiba ya nchi, lakini bado wanaendelea kuwapo bungeni bila ya kuwa na chama," alisema.

Alisema hivi karibu mmoja kati ya wabunge hao 19, Jesca Kishoa, akichangia mjadala bungeni, alikiri mwenyewe kwamba wamefukuzwa uanachama, lakini Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson, alimtaka mbunge huyo kufuta kauli yake hiyo kwa kuwa Bunge halina taarifa hiyo.

"Wabunge wenyewe wanajisema kuwa wamevuliwa uanachama, lakini bado Spika na Naibu wake wanadai Bunge halina taarifa ya kuvuliwa kwao, huku siyo kutenda haki kwa vyama vya upinzani," alisema.

Alisema kuwa baraza hilo linao ushahidi kuwa barua za kuvuliwa uanachama kwa wabunge hao zilimfikia Spika Ndugai ofisini kwake.

"Hapa tunacho kitabu cha makabidhiano ambacho kinaonyesha kuwa barua iliyo andikwa na Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, ya kumweleza Spika Ndugai kuwa wabunge hao wamevuliwa uanachama, ilipokelewa na kutiwa saini na mmoja wa watumishi wake," alisema Ruge.

Pia, alisema kuwa pamoja na ushahidi wa kitabu hicho cha makabidhiano, wanao ushahidi wa barua zilizotumwa kupitia DHL, ambazo zilimfikia Spika.

Ruge alisema ni wakati sasa kwa Spika Ndugai kujitokeza hadharani kukanusha kama kweli hajawahi kupata barua hizo.



Baadhi ya wanafunzi wa vyuo vikuu, kikiwamo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), wakimsikiliza mtaalamu wa maji, Mhandisi David Munkyala (katikati), walipotembelea mradi wa bwawa la kufua umeme la Mwalimu Nyerere, Rufiji mkoani Pwani, ili kujifunza na kujionea maendeleo ya mradi huo. **PICHA: MARGARET MALISA**

# Wanaharakati wamwomba Katiba Mpya Rais Samia

**Na Christina Mwakangale**

WANAHARAKATI na wadau wa haki za binadamu nchini, wamemwomba Rais Samia Suluhu Hassan kuurudisha mchakato wa upatikanaji wa Katiba mpya, wakidai kuwa ya sasa haikidhi vigezo kwenye baadhi ya vipengele.

Kwa kuzingatia kwamba Rais Samia alikuwa Makamu Mwenyekiti wa Bunge la Katiba, wadau hao walimwomba Mkuu wa nchi huyo akumbuke umuhimu wa upatikanaji wa Katiba Mpya ili kuendana na matakwa ya nchi.

Rai yao hiyo waliitoa juzi wakati wa mdahalo wa wazi kwa ajili ya kukuza uelewa kwa Watanzania kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu mchango wa katiba katika kukuza na kustawisha uhuru na maendeleo.

Katika mdahalo huo, baadhi ya washiriki walisema katiba ya mwaka 1977 haina uwakilishi wa wananchi na imetoa mamlaka makubwa kwa baadhi ya watendaji wa serikali.

Salvatory Magafu, Mkurugenzi wa Sheria na Haki za Binadamu, aliyemwakilisha Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (CUF), Profesa Ibrahim Lipumba, alisema katiba iliyopo haikidhi maisha ya sasa ya Watanzania.

Magafu, akizungumzia historia ya katiba tangu uhuru na mustakabali wake, yakiwamo mabadiliko ya sayansi, uchumi na siasa, alisema haikidhi na inahitaji mabadiliko.

Alisema kuwa baada ya uhuru, Watanzania wengi hawakuhusishwa katika kuaanda katiba ya nchi, badala yake walihusishwa wabunge wachache.

"Katiba ilipitisha Rais kuwa kiongozi wa Mkuu wa Serikali, Amiri Jeshi Mkuu na mwenye mamlaka makubwa. Mwaka 1964 baada ya kupatikana Katiba ya Muungano pamoja na kwamba ilikuja mwaka 1965, haikusaidia kushirikisha Watanzania," alisema.

Magafu alisema Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, iliyoongozwa na Shehe Thabit Kombo na tume kupewa kazi ya kuiandaa ikiwa na wajumbe 20 kutoka pande zote mbili, 10 kutoka bara na 10 visiwani, nayo ina upungufu.

"Urais wa kifalme, chama kimoja cha siasa, katiba hii ilipita na imefanyiwa marekebisho mara 14, ambayo tuliirithi kutoka mkoloni.

"Mwaka 1992 (Ali Hassan) Mwinyi aliiunda Tume ya Nyalali, kwamba sheria kandamizi ziondolewe ambayo ni mapendekezo, hayakufanyiwa kazi zaidi ya pendekezo pekee la kuondolewa chama kimoja.

"Tume ya (Mabadiliko ya Katiba) iliundwa na JK (Jakaya Kikwete) mwaka 2012, katiba ikajadiliwa kupitia Bunge la Katiba, lakini hatua za mwisho hazikufikiwa.

Kilikuwa kipindi pekee ambacho tungepata katiba ya wananchi, hii katiba ya sasa inashindwa kutetewa, wananchi wanaitaka rasimu ya (Jaji Joseph) Warioba.

Magafu alishauri kuwa ama ichukuliwe rasimu aliyoianzisha Jaji Warioba au mchakato mpya uanzishwe ambao hata hivyo anaona utakuwa na gharama kubwa.

Alisema mamlaka ya kuigawa nchi, yana mgongano katika katiba zote mbili na kwamba Rais wa Tanzania ndiye mwenye mamlaka ya kuigawa Tanzania baada ya kushauriana na Waziri Mkuu, huku Rais wa Zanzibar akitakiwa kushauriana na Rais wa Tanzania.

Magafu alisema mkanganyiko huo unaweza kubadilika iwapo katiba itafanyiwa marekebisho na kwamba kwa kuzingatia Rais Samia ndiye alikuwa Makamu Mwenyekiti wa Bunge la Katiba, aukumbuke mchakato wa kupata Katiba Mpya.

Wakili wa Kujitegemea, Mhadhiri na Mtetezi wa Haki za Binadamu, Harold Sungusia, alisema ili kuwapo mgawanyo mzuri wa madaraka kati ya Serikali, Bunge na Mahakama, nchi inahitaji kuwa na Katiba Mpya.

Alisema katiba iliyopo ina nadharia ya suala hilo na ilirithiwa kutoka kwa mkoloni, Alisema upatikanaji wa Katiba ya Jamburi ya Muungano wa Tanzania na malengo yake ulikuwa na tatizo kutokana na ushiriki duni wa wananchi.

"Haki za Muungano ziwekwe wazi na zijulikane katika Makumbusho ya Taifa ili kila mmoja ajue Muungano huu mzuri ambao ni wa kipekee barani Afrika uliodumu Afrika," alisema.

Alisema muundo wa muungano ndiyo unaleta mkwamo wa kuipata Katiba Mpya na kwamba washiriki wa upatikanaji wa Katiba Mpya wasiwe wagombea wa nafasi za kisiasa.

Sungusia alionya kuwa kuwaweka wanasiasa kunaleta mgongano wa kimaslahi.

Awali, akifungua mdahalo huo uliokutanisha washiriki mbalimbali kwa njia ya mtandao, Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, alisema mdahalo huo ni msingi na elimu ambayo imekuwa ikitolewa na kituo hicho.

Henga alisema kituo hicho kiliandaa mdahalo wa wazi kwa ajili ya kukuza uelewa kwa Watanzania kwenye mambo mbalimbali yanayohusu mchango wa katiba katika kukuza na kustawisha uhuru na maendeleo yao.

Mwanazuoni, Mwandishi na Mtetezi wa Haki za Binadamu, Dk. Ananilea Nkya, alisema katiba ya sasa ina tatizo katika mamlaka ya Rais kwenye uteuzi, akigusia kuwapo ukakasi katika kuzingatia usawa wa kijinsia kwenye uongozi.

Alisema mamalaka ya juu ya Rais inafanya kupatikana viongozi wasio na sifa na weledi na kutokubalika kijamii.

"Ari ya viongozi wa kuchaguliwa yaani wabunge, madiwani hukwamishwa na viongozi wa wilaya. Mamlaka ya Rais kuteua kila mtu, wapo baadhi ambao hawana sifa, baadhi hawana uadilifu, fursa tu aliipata ya uteuzi.

"Utakuta kiongozi anaapa kwa kufuata katiba lakini utakuta anafanya kazi ili kumfurahisha aliyemteua kuliko jamii, yote inatokana na kurithi katiba ya kikoloni.

"Nchi hii ina wanawake wengi lakini katiba haijaainisha suala la kijinsia, tunahitaji katiba mpya, ukiangalia Bunge lililopita lilikuwa na wabunge 393, lakini wengi ni wanaume.

"Rasimu ya Warioba iliweka usawa wa kijinsia, kwamba itakuwa asilimia 50/50 kwa wabunge wote na idadi itapungua, tuna wabunge wengi na gharama kubwa," alisema Nkya.

# Kampeni kunawa mikono yaja

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya My Legacy kwa kushirikiana na Habitat For Humanity, wameanzisha kampeni ya Nawa Mikono Kwa Afya, yenye lengo la kutoa elimu ya usafi katika shule za msingi na sekondari, masoko, migahawa na jamii kupitia watendaji wa serikali za mitaa.

Kampeni hiyo itakayozinduliwa mapema mwezi ujao, italenga kutoa vifaa vya kunawia mikono, sabuni na kutoa elimu kwa jamii ili kujenga utamaduni wa kuzingatia kanuni za afya kujikinga na maradhi yanayoambukiza vikiwamo virusi vya corona (Covid-19).

Akizungumza na waandishi wa habari juzi jijini Dar es Salaam wakati wa kutambulisha mradi huo wa miaka mitano, Mkurugenzi wa My Legacy, Fortunata Temu, alisema watanunua vifaa ambavyo vitawekwa katika maeneo ya shule, masoko, vituo vya daladala na kwenye migahawa.

"Lengo la kampeni yetu ni kufikia watu wa ngazi mbalimbali. Kuna shule ambazo zina wanafunzi zaidi ya 1,000 hadi 2,000 ambazo zipo pembezoni na hazifikiwi na huduma kama hizi, nazo tutaweka vifaa hivyo vitawasaidia," alisema Temu.

Alisema Taasisi ya Habitat for Humanity inayohusika na uboreshaji wa makazi ya watu, watashirikiana nayo kutekeleza mradi huo ili kuhakikisha makazi yanakuwa safi na salama.

Mratibu wa mradi huo, Yasinta Mtavangu, alisema kuwa katika hatua za mwanzo, wataanza na Mkoa wa Dar es Salaam, ambako wanatarajiwa kuzifikia kata za Kawe, Kunduchi na Wazo Hill wilayani Kinondoni.

Alisema kuwa kabla ya kuchagua kata hizo, walifanya utafiti na kubaini kuwapo kwa uhitaji katika shule nane zikiwamo za msingi nne na sekondari nne ambazo zitanufaika na mradi.

Mtavangu alizitaja shule zitakazonufaika kuwa ni pamoja na Sekondari ya Twiga na Shule za Msingi Kisauke na Kawe Mkwamani.

Alisema wanafunzi watapewa elimu ya kutengeneza sabuni zao wenyewe ili kuendeleza mradi huo wa kunawa mikono.

Alisema watafika katika Soko la Tegeta Nyuki na Kawe ambako nako kuna uhitaji mkubwa wa elimu ya usafi na uhaba wa



Mkurugenzi wa kampuni ya Bravo Agency, Abbasi Mtemvu, akikabidhi msaada wa vyakula mbalimbali kwa watu wenye ulemavu, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE**

# Auawa na wanafunzi akidaiwa kuiba godoro

**Na Said Hamdani, LINDI**

WATU wawili wakazi wa Wilaya za Lindi na Ruangwa mkoani Lindi, wamepoteza maisha katika matukio mawili tafauti, likiwamo la kukanyagwa na tembo walioingia shambani.

Mbali na tembo, mmoja wao anadaiwa kuuawa na wanafunzi wakimtuhumu kuingia shuleni kinyume cha taratibu na kuiba godoro.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Mtatiro Kitinkwi, wakazi hao walifikwa na umauti huo Aprili 19 na 21 mwaka huu.

Aliwataja waliofikwa na umauti kuwa ni Mohamed Kumtunga (60), mkazi na mkulima wa Tarafa ya Milola na Udongo Nguruwe (19) wa Kata ya Mbekenyera wilayani Ruangwa.

Kitinkwi alisema Kumtunga aliuawa kwa kukanyagwa na kundi la tembo Aprili 19 mwaka huu majira ya saa 12:30 jioni alipokuwa anawafukuza wanyamapori hao walipoingia shambani kwake kula mazao.

"Huyu Kumtunga alikuwa anafukuza tembo walioingia Shambani kula mazao yake, ndipo akashambuliwa na kupoteza uhai wake," alisema.

Kamanda huyo alisema Nguruwe amekufa kutokana na kushambuliwa na wanafunzi alipokuwa akiiba godoro kwenye bweni linalotumiwa na wanafunzi wanaosoma Shule ya Sekondari Mbekenyera Aprili 21, mwaka huu majira ya saa tatu asubuhi.

Alibainisha kuwa Nguruwe baada ya kupigwa na wanafunzi hao, alipelekwa katika Hospitali ya Wilaya ya Ruangwa, ambako alifariki dunia wakati akipatiwa matibabu.

"Siku hiyo huyu Nguruwe alikuwa ameingia moja ya mabweni ya wanafunzi na kuiba godoro, alipokuwa anatoka nalo nje, akakumbana na kichapo," alisema Kamanda Kitinkwi.

Kamanda huyo alisema hakuna mwanafunzi aliyekamatwa kuhusiana na mauaji hayo, lakini wanaendelea kufanya uchunguzi kubaini wahusika ili sheria ichukue mkondo wake.

Aliionya jamii kutojichukulia sheria mikononi pale inapokamata mhalifu badala yake ihakikishe inamfikisha Kituo cha Polisi kwa hatua zaidi.

# JKT waokoa bilioni 8/- umwagiliaji

**Na Renatha Msungu, MLIMBA**

JESHI la Kujenga Taifa (JKT) limeokoa Sh. bilioni nane katika ujenzi wa skimu ya umwagiliaji ya mashamba ya mpunga eneo la Chita mkoani Morogoro baada ya kutumia wataalamu wa ndani wa jeshi hilo na vijana wa kujitolea.

Imebainishwa kuwa kimu hiyo ingegharimu Sh. bilioni 12 kama wangetumia makandarasi kutoka nje, lakini ujenzi huo hadi unakamilika utagharimu Sh. bilioni nne kwa kutumia wataalamu wa ndani ya jeshi.

Akizungumza wakati wa ziara ya kukagua maendeleo ya mradi huo jana, Kaimu Kamanda wa Kikosi 837 Chita JKT, Meja Evergreen Bartazal, alisema skimu hiyo ikikamilika, itasaidia kumwagilia ekari nyingi za mpunga ambazo zinatarajiwa kulimwa katika msimu ujao wa kilimo.

"Hii Skimu itasaidia sana katika kilimo cha umwagiliaji wa mashamba ya mpunga, lakini pia jamii inayozunguka eneo hili itanufaika na bwawa hilo," alisema.

Meja Bartazal alibainisha kuwa mwaka jana baada ya kupata fursa ya kujengewa mradi huo ambao hivi sasa unaendelea na ujenzi wake, waliendelea na mpango wa kuendesha kilimo mkakati ili kuhakikisha wanafikia malengo waliojiwekea.

Alisema tayari wamepanda ekari 150 za mbegu za mpunga ambazo zitatosheleza kupanda katika mashamba ya jeshi hilo na mbegu nyingine zitasambazwa kwa jamii inayozunguka maeneo hayo.

Meja Mbaraka Magogo, Makamu Kamanda wa Operesheni ya Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji katika Shamba la Chita, alisema wameshirikiana na wataalamu kutoka Tume ya Umwagiliaji.

Alisema tayari wameshatengeneza mabanio kwa ajili ya kufungua maji na kufunga pale yanapohitajika kuelekezwa shambani.

Meja Magogo alisema hivi sasa ujenzi huo unaendelea vizuri kutokana na ushirikiano wa wataalamu ambao wamejipanga vizuri kuhakikisha skimu ya hiyo inakamilika.

Alisema shamba la mpunga katika eneo hilo limeandaliwa kisasa kupitia wataalamu wa kilimo waliopo ndani ya jeshi kuhakikisha linakuwa shamba darasa kwa jamii.

Kijana wa Kujitolea, Barkat Mlugu, alisema mafunzo ya JKT yamemjengea uwezo kujitegemea katika kilimo atakapomaliza mafunzo yake.

Alisema kuwa akiwa uraiani, atatumia elimu aliyoipata kuwafundisha vijana wengine wa mtaani ambao hawajapata nafasi ya kujiunga na jeshi hilo.

000000

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tahadhari kuhusu maafa hazina budi kuzingatiwa

**WANANCHI** wa maeneo ya mwambao wa pwani ya Tanzania husasan Dar es Salaam, Mtwara, Pwani, Lindi na visiwa na Mafia na Zanzibar wako katika hofu kutokana na tishio la kimbunga Jobo ambacho tayari kimeshaleta maafa katika nchi jirani ikiwamo Msumbiji.

Hadi jana ilielezwa kuwa kimbunga hicho kilikuwa umbali wa takriban kilomita 200 kutoka kisiwa cha Mafia licha ya kwamba wataalamu wa hali ya hewa walitoa taarifa kwamba kilikuwa kinapungua nguvu. Pia wataalamu hao walibainisha kuwa kimbunga hicho kinatarajia kuingia nchini kikiambatana na mvua kubwa.

Kutokana na kuwapo kwa tishio hilo, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imeendelea kuwataka wananchi katika mikoa ya ukanda wa pwani ya bahari ya Hindi kuchukua tahadhari wakati kimbunga hicho kikitarajiwa kufika kwenye maeneo hayo kesho.

Mamlaka hiyo ilibainisha kwamba ingawa kimbunga hicho kinazidi kupungua nguvu kadri kinavyokuja, bado tahadhari lazima zichukuliwe kutokana na taarifa za kitaalam kwamba mpaka kufika Dar es Salaam, kitakuwa na nguvu ya kasi ya kilomita 60 kwa saa. Sambamba na upepo mkali wa kilomita 50 mpaka 60 kwa saa.

Kama ilivyoeleza mamlaka hiyo, wananchi wanapaswa kuwa katika tahadhari kwa kuwa maafa yanaweeza kutokea kama ambavyo iliwahi kutokea katika vimbunga vingine vilivyotangulia kama vile tsunami.

Tunasisitiza tahadhari zinapaswa kuchukuliwa kwa sababu mara kwa mara, katika maeneo mbalimbali, wananchi wamekuwa wakipuuza tahadhari zinazotolewa na taasisi mbalimbali za serikali au maagizo ya kutakiwa kujilinda na magonjwa ya mlipuko.


Katika maafa yaliyotokea mwanzoni mwa miaka ya 2010 kutokana na mvua kubwa, wananchi katika maeneo mbalimbali waliathiriwa ikiwamo kupoteza maisha na mali zao. Sababu kubwa ilikuwa kupuuza au kutokuzingatia tahadhari zilizotolewa.

TMA, katika maafa hayo ambayo yalisababisha vifo, wanyama kusombwa na nyumba na mali mbalimbali kuharibiwa, ilitoa tahadhari na kuwataka watu kuhama mambondeni lakini hawakufanya hivyo. Matokeo yake mvua kubwa ilinyesha usiku na kuharibu miundombinu ya usafirishaji. Katika jiji la Dar es Salaam, kwa mfano, makazi ya watu maeneo ya mabondeni yaliharibiwa na baadhi ya watu kupoteza maisha.

Mfano mwingine ni wakati wa janga la corona mwaka jana. Kutokana na tatizo hilo, serikali iliagiza watu kuzingatia kanuni za afya ikiwamo kukaa umbali wa mita moja kutoka mtu mmoja hadi mwingine lakini baadhi ya watu waliendelea kutozingatia maagizo hayo. Hatua hiyo iligharimu maisha ya watu kadhaa kwenye maeneo mbalimbali ya nchi.

Kwa mifano hiyo michache, ni dhahiri kwamba jamii inakumbuka maafa yaliyotokea katika vipindi hivyo. Kwa mantiki hiyo, kwa tishio ambalo limetangazwa kutokea nchini, Watanzania tunapaswa kuchukua tahadhari kwa kuzingatia maelekezo yaliyotolewa.

Kama wahenga wasemavyo tahadhari kabla ya hatari, ni vyema kila mtu akazingatia maagizo ya serikali kupitia TMA. Ni imani kwamba kwa kufanya hivyo, hakuna maafa makubwa yanayoweza kuipata Tanzania.




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Huduma nzuri DAWASA zisiharibiwe na watumishi wenye lugha za maudhi

**MAJI** ni rasilimali muhimu kwa maisha ya viumbe vyote na maendeleo ya kiuchumi na kijamii, na pia ubora wa afya na wa mazingira vinategemea kuwapo kwa maji ya kutosha na yenye ubora unaotakiwa.

Vilevile, bila maji hakuna maisha, kutokana na umuhimu wake, ndiyo maana mamlaka zinazohusika na usimamizi wa maji, zimekuwa zikifanya kila liwezekanalo ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma hiyo.

Kimsingi ni kwamba, ukosefu wa maji safi na salama kwenye baadhi ya maeneo, ni kero, kwa kuwa unasababisha watu kutembea umbali mrefu kufuata huduma kwa kuwa ni ya muhimu.

Kwa upande wa Jiji la Dar es Salaam, Mamlaka ya Maji safi na Majitaka Dar es Salaam (DAWASA), imekuwa na mikakati mbalimbali ya kusogeza huduma ya upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi wa jiji hilo.

Miongoni mwa mikakati hiyo ya DAWASA, ni utekelezaji wa miradi mikubwa, uboreshaji na usambazaji wa maji kwenye maeneo yenye huduma hiyo imekuwa ikipatikana kwa shida.

Hatua hiyo inalenga kampeni ya 'Kumtua mama ndoo kichwani', na kwamba, mamlaka hiyo imeamua kuhakikisha asilimia 35 ya mapato yake ya ndani yanakwenda kutekeleza ujenzi wa miradi mikubwa ya kusambaza huduma ya maji kwenye maeneo ambayo hayana maji.

Miradi mingine ni ule wa uboreshaji usambazaji wa maji kutoka Makongo hadi Bagamoyo mkoani Pwani, wenye thamani ya Sh. bilioni 65 na ule wa Kisarawe hadi Pugu.

Kwa ujumla ni kwamba, DAWASA imedhamiria kutekeleza miradi mikubwa, uboreshaji na usambazaji wa kwenye maeneo yote yenye uhaba wa huduma hiyo muhimu katika maisha ya binadamu na viumbe vingine.

Juhudi zinazofanywa na DAWASA ni za kuunga mkono, lakini pamoja na hayo, kuna baadhi ya watumishi, ambao kwa namna moja au nyingine wanaweza kuiharibia mamlaka hiyo mbele ya umma.

Kwenye baadhi ya ofisi za mamlaka hiyo, wapo watumishi ambao wakati mwingine wanakatisha tamaa, kwa kutokuwa na lugha rafiki kwa wateja, kana kwamba hawajafundishwa jinsi ya kuhudumia wateja.

Aidha, wengine hawafiki ofisini kwa wakati na hata kutopokea simu za wateja pale wanapotafutwa na pia kutotoa vifaa kwa ajili ya kuunganishiwa maji kwa visingizio mbalimbali.

Mteja anaweza kwenda kwenye baadhi ya ofisi za mamlaka hiyo kuhitaji vifaa vya kuunganishiwa maji na kuambiwa kuwa mtunza stoo hayupo, hali ambayo inakwamisha wateja kupata huduma hiyo kwa wakati.

Ni vyema viongozi wakafuatilia hilo kwenye ofisi mbalimbali za mamlaka hiyo kuona utendaji wa baadhi ya watumishi, ili kuondoa kero hiyo ambayo inachangia kukatisha tamaa wateja.

DAWASA ina kaulimbiu isemayo 'Tunawahitaji', ambayo kama sikosei, maana yake ni kwamba mamlaka hiyo inahitaji wateja, hivyo ni vyema wakahudumiwa kwa wakati na tena kwa lugha rafiki.

Kwa kawaida lugha nzuri huvutia wateja na hata kuwa na imani na huduma wanayopewa hata kama itakuwa ni ahadi, lakini watumishi wanapotumia lugha mbaya, maana yake ni kwamba, wanaiharibua mamlaka hiyo.

'Tunawahitaji' ndiyo kaulimbiu ya DAWASA, hivyo si vibaya watumishi wakawafanya wateja kama wafalme ili wafurahie hudunma badala ya watu wachache hao kuivurugia mamlaka hiyo.

Lugha nzuri ya kumkaribisha mteja pamoja na huduma bora, ni mtaji mkubwa katika biashara, kwa kuwa vinaweza kumfanya mtu akawa mteja wa kudumu, kutokana na jinsi anavyohudumiwa.

Hivyo, baadhi ya watumishi ambao wamekuwa wakitumia lugha mbaya au kutotoa huduma kwa wakati, wanaweza kuchangia kuifanya mamlaka hiyo ionekane haifai mbele ya jamii na kumbe wachache tu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

SAFU

AFYA

# Siri iliyojificha manufaa ya iliki kwa afya ya binadamu



**Na Mwandiashi Wetu**

ILIKI ni kiungo maarufu duniani hasa katika nchi za Asia kutokana na kutumiwa katika kuongeza ladha katika vyakula na vinywaji mbalimbali pamoja na dawa.

Umaarufu wa kiungo hiki umezidi kuongezeka mwaka hadi mwaka duniani hasa kutokana na uzuri wa harufu na ladha yake.

Inadaiwa kuwa katika miaka ya sasa, matumizi ya iliki katika vyakula ni mengi na inakadiriwa kuwa takriban asilimia 99 ya watu duniani wanatumia sana kiungo hiki lakini wengi hawajui kuwa mbali na kwamba ni kiungo katika chakula, kuna faida nyingi za kiafya.

Kwa ujumla, iliki ni chanzo kizuri cha madini mwilini kama vile madini ya potasiamu, kalsiamu, salfa, chuma na maganizi. Pia iliki ina utajiri wa vitamini nyingi ambazo ni muhimu sana kwa afya ya mwili. Vitamini zinazopatikana katika iliki ni pamoja na A, B na C, Niacin na Riboflavin.

Kutokana na wingi wa madini na vitamini, iliki ina faida zifuatazo katika mwili wa binadamu;-

**KUONDOA HARUFU**

Iliki ina msaada mkubwa katika afya ya kinywa na meno kutokana na uwezo wake mkubwa katika kuondoa harufu mdomoni. Inaelezwa kuwa kiungo hicho, kina viashiria ambavyo vinaweza kuuwa vijidudu vinavyosababisha harufu mbaya katika kinywa.

Sambanba na hilo, iliki husaidia kutibu magonjwa ya meno na kuua bakteria na wadudu walioko katika meno na hatimaye kuimarisha afya ya kinya na meno.

Ili kufanikisha hilo, mtu anashauriwa kutafuna iliki kila baada ya mlo ili kuacha kinywa kuwa safi na harufu nzuri. Pia anashauriwa kusukutua kinywa kwa maji ya vuguvugu ya iliki mara mbili kwa siku ili kuondoa tatizo la harufu katika kinywa.

**USAGAJI CHAKULA**

Iliki ni muhimu katika kuimarisha afya ya mfumo wa kusaga na kusharabu chakula na pia inachochea uzalishaji wa nyongo kwa ajili ya kuyeyusha vyakula vyenye mafuta mengi mwilini.

Hali hiyo pia husaidia kupunguza gesi tumboni, kuondoa kiungulia na kutibu maumivu ya tumbo. Ili kuwezesha mfumo huo kufanya vizuri, mtu anashauriwa kuweka iliki katika vyakula au kunywa sana chai ya iliki.

**KUONGEZA HAMU YA KULA**

Kutokana na uzalishaji wa nyongo kwa ajili ya kunyeyusha vyakula vya mafuta na virutubisho vingine ambavyo vinachangia kuondoa hamu ya kula, inaelezwa kuwa matumizi ya iliki mara kwa mara katika vyakula husababisha mtu kuwa na hamu ya kula, hivyo kuimarisha afya ya mwili.

Katika kufanya hivyo, inashauriwa kuweka unga wa iliki katika supu au kutafuna mbegu zake.

**MZUNGUKO WA DAMU**

Wataalamu wa tiba wanabainisha kuwa matatizo ya mzunguko wa damu mwilini yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka kutokana na mtindo wa maisha pamoja na maradhi mbalimbali yakiwamo ya moyo.

Hata hivyo, wataalamu wanaeleza kuwa iliki inasaidia kuimarisha mzunguko wa damu kwenye mapafu na kuzibua mirija ya hewa hivyo kuwapa unafuu wenye matatizo ya pumu na matatizo mengine ya upumuaji.

**MAUMIVU YA KICHWA**

Iliki huondoa maumivu ya kichwa yanayotokana na tatizo la usagaji wa chakula.

Kunywa kikombe kimoja cha chai ya hiriki kuondoa maumivu ya kichwa.

**TIBA NJIA YA MKOJO**

Watu wengi wamekuwa wakikabiliwa na maradhi mbalimbali ya njia ya mkojo ikiwamo UTI. Habari njema ni kwamba iliki ina msaada mkubwa katika kupambana na maradhi hayo .

**MAFUTA KWENYE MISHIPA**

Kutokana na mfumo wa maisha hasa ulaji wa yakula vvyenye mafuta, watu wamekuwa wakiathiriwa na maradhi mbalimbali yakiwamo ya mishipa.

Sasa hii ni habari njema kwa watu wanaosumbuliwa na hatizo hilo, kwani imeelezwa kuwa iliki husaidia kuondoa mafuta kwenye mishipa na hatimaye kuwafanya watu kuwa na afya njema.

**MSONGO WA MAWAZO**

Tatizo la msongo wa mawazo limekuwa likiongezeka katika jamii kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo watu kutokufikia ndoto zao, kuzidiwa na majukumu au kutendwa na watu wa karibu yao.

Hatua hiyo kusababisha maradhi kama vile ya moyo, kisukari, shinikizo la damu, kiharusi na hata kupoteza maisha.

**Imeelezwa kuwa matumizi ya iliki mara kwa mara yanapunguza tatizo la msongo wa mawazo.**

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Tuwe na Rais Samia si Mama Samia



**Na Joseph Kulangwa**

**Mwalimu alisema: "Siku moja nikamtuma Sir George kwenda Congo. Alipanda ndege, basi ndege ile ikakumbana na dhoruba angani, iliporuka juu akasema 'my God', ikaruka tena akasema 'Mungu Wangu' safari ya tatu ikaruka juu zaidi, akasema 'maweeee'!**

MTOTO anapoanza kujifunza kutamka maneno, mara nyingi neno 'mama' humjia haraka na kirahisi, na kila apatapo shida, huita mama. Hata siku moja hutamsikia kuita baba.

Anamwona mama kuwa ni kila kitu maishani mwake, na ndiye anayeweza kumsaidia kutatua kila tatizo alilonalo, hata kama hajui tatizo ni nini, pengine hiyo inatokana tu na jinsi ya maumbile na uumbaji wa Mungu.

Haishangazi pia, kusikia jitu zima au zee zima, linapopatwa na matatizo, kuita mama. Si mara moja au mbili, mtu mzima akipatwa na ajali mathalan, utasikia analia "mama weee!"Haishangazi mtu kushitukia jambo ukamsikia akiita "mama yangu!"

Nakumbuka siku moja mwaka 1995 pale hoteli ya Kilimanjaro, Dar es Salaam, Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere akizungumza na wanahabari, alichomekea utani kuhusu mtani wake, Sir George Kahama aliyepata kuwa mmoja wa mawaziri wa kwanza katika serikali yake.

Mwalimu alisema: "Siku moja nikamtuma Sir George kwenda Congo. Alipanda ndege, basi ndege ile ikakumbana na dhoruba angani, iliporuka juu akasema 'my God', ikaruka tena akasema 'Mungu Wangu' safari ya tatu ikaruka juu zaidi, akasema 'maweeee'!

Mawe kwa Kihaya ni mama yangu. Sasa kwa umri wa Mzee Kahama, kulia mama yangu ina maana kubwa, kwamba kwa kweli mama ni mama na mama ni kila kitu katika maisha ya binadamu. Hutasikia baba yangu au baba wee au tateee!

Lakini hata katika kutukana, utasikia watu wanatukanana kwa kutumia majina ya mama, wakiamini kwamba mtu ukimtukania mama yake ndipo utakuwa umempata na umemuumiza. Watu hawajali kuwatukania baba zao, hata siku moja. Hapana haja ya kujiuliza, ila ndivyo ilivyo.

Inabaki kuwa ukweli tu, kuwa mama ni roho ya familia na bila mama familia inayumba. Mtu akimwona mama yake yupo, hata kama mtu huyo ni mzee kiasi gani, hupata faraja ya moyo na kujiona yuko salama.

Watanzania hivi sasa tumempata mama. Tuna kiongozi mmama. Tuna Rais wa Jamhuri mmama au mwanamke. Ndiyo sababu watu wanamwita Mama Samia Suluhu Hassan. Wakifupisha, utawasikia wakisema Mama kasema, au Mama Samia kasema. Mama Samia kanguruma, nakadhalika.

Utawasikia watu katika kona mbalimbali, wakitamba, kuwa Tanzania sasa imepona kwa sababu imepata mama. Utasikia kuwa hotuba za Mama zinatia faraja. Tanzania imerejeshewa furaha, kutokana na hotuba za Mama.

Wapo wengine wanaosema Mama Samia ni sawa na muuguzi, anakuchoma sindano huku akikwambia pole. Mama Samia anang'ata na kupuliza, hivyo hupati maumivu hata kama anakupiga dongo! Wanasenma Mama Samia hafoki, lakini anakupa makavu.

Mama Samia, kama watu wanavyomwita sana, amekuwa muwazi na anataka Tanzania isonge mbele, anataka ya nyuma yasiyo mema yaachwe na tugange mema yajayo, anataka kuonana na kila kundi nchini, ili kujua linafikiria nini, na nini kifanyike nchi isonge mbele.

Kaingia na mguu mzuri, kapokewa na mkono mzuri na wananchi. Bila shaka kazi iliyoanzishwa na hapa kazi tu itaendelea, lakini pengine kwa mtindo tofauti na wa Hapa Kazi Tu, ili mradi ikiwa na lengo zuri la kumsaidia Mtanzania.

Lakini pamoja na kwamba tunatambua ni mama au kama apendavyo kusema yeye ni Rais katika maumbile ya mwanamke, bado anastahili kutambulishwa kama Rais Samia Suluhu Hassan na si marazote kumtambulisha kama Mama Samia, kwa sababu huko nyuma hatukupata kuwatambulisha viongozi wetu hivyo.

Sikumbuki kumtambulisha Baba Julius Kambarage Nyerere, Baba Ali Hassan Mwinyi, Baba Benjamin William Mkapa, Baba Jakaya Mrisho Kikwete au Baba John Pombe Magufuli, ila Rais fulani, fulani, fulani, fulani, fulani.

Ili kumtofautisha na kina mama wengine, tuache kumwita mama au wengine wakimwita Bi Mkubwa, bali tujikite katika kumtambulisha kwa wadhifa wake na kumpa heshima stahiki, miongoni mwa marais wenzake Afrika na duniani.

**Alamsiki!**

## KONA YA UKWELI

# Sheria sasa ifuatwe uhalali kina Mdee kuwapo bungeni



Na Thobias Mwanakatwe

**Sheria zilianza kukiukwa na Spika wa Bunge la Tanzania, Job Ndugai, ambaye alisema wabunge 19 walioteuliwa na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kwa ajili ya viti maalumu na kisha kuapishwa ni wabunge halali isipokuwa wao wenyewe waamue vinginevyo!**

HISTORIA ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilianza mara baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Aidha, Bunge la Tanganyika lilianza Machi 19, 1926 siku ambayo Bunge la Uingereza lilipitisha Sheria iliyoitwa "The Tanganyika (Legislative Council) Order in Council, 1926" Kipindi hicho likijulikana kama Baraza la Kutunga Sheria la Tanganyika.

Tanganyika wakati huo ilikuwa chini ya utawala wa Uingereza ambayo ilikuwa imepewa mamlaka na Umoja wa Mataifa kuisimamia Tanganyika hadi ipate uhuru wake. Sheria hiyo ambayo ilitaka kuanzishwa Baraza la Kutunga Sheria, ilichapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 18 Juni, 1926. Baraza hilo liliitwa "The Legislative Council of Tanganyika Territory" na kujulikana zaidi kwa kifupi kama "LEGCO".

Sheria zote zilizokuwa zikitungwa na Baraza hili zilikuwa zinapelekwa Uingereza kwa ajili ya kupata idhini ya Mkuu wa Nchi kabla ya kuanza kutumika.

Kutokana na sheria zilizopo, ili kuwa mbunge wa kuchaguliwa au mbunge wa viti maalum sharti mojawapo ni lazima utokane na chama cha siasa. Lakini pia idadi ya wabunge wa viti maalum hutokana na idadi ya kura walizopigiwa wabunge wote wa chama husika waliosimamishwa majimboni hata kama hawakushinda. Chama kinachopata walau asilimia tano ya kura zote ndicho hukidhi vigezo kutoa majina ya wabunge wa viti maalum.

Na huu utaratibu wa viti maalum vya wanawake unapatikana katika nchi mbalimbali na unalenga kuongeza idadi ya wanawake na athira yao katika bunge na mabaraza kwa hiyo katika siasa kwa jumla ya nchi.

Utaratibu wa kupata wabunge wa viti maalum ulianza kufinyangwa kwa kutozingatia sheria hali ambayo ilizua taharuki ndani na nje ya nchi mara tu baada ya uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 28, 2020.

Sheria zilianza kukiukwa na Spika wa Bunge la Tanzania, Job Ndugai, ambaye alisema wabunge 19 walioteuliwa na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kwa ajili ya viti maalumu na kisha kuapishwa ni wabunge halali isipokuwa wao wenyewe waamue vinginevyo!

Kauli hiyo ya Spika ilizua sintofahamu kuhusu wabunge hao wa viti maalum kwasababu sheria ilikuwa imekiukwa.

Kukiukwa kwa sheria, kulitokana na kwamba wakati spika Ndugai akitangaza kuwatambua wabunge hao, Kamati Kuu ya CHADEMA ilikuwa imechukua uamuzi wa kuwafutia uanachama wabunge hao wakiongozwa na aliyekuwa mbunge wa Kawe na Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake CHADEMA (BAWACHA), Halima Mdee.

Lakini wakati Spika Ndugai akikiuka sheria katika jambo hilo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wanasheria wengine wa nchi hii walikaa kimya pasipo kulipigia kelele, jambo ambalo kimsingi ni aibu kwa taifa.

Nimeibuka kuandika jambo hili hasa baada ya Jumanne wiki hii, Rais Samia Suluhu Hassan, alipoonekana katika vyombo vya habari na mitandao ya kijamii akiteta jambo na Spika Ndugai ikiwa ni siku mbili kabla ya kulihutubia Bunge.

Japo haikufahamika walichojadiliana, ningetamani kama suala hilo la wabunge wa viti maalum wa CHADEMA lingekuwapo katika mazungumzo yao maana limeleta ukakasi na aibu kubwa kutokana na kufinyangwa kwa sheria.

Kwa kuwa sasa tupo katika utawala wa awamu ya sita chini ya Mama Samia, ni wakati sasa sheria ifuatwe ili wabunge wa viti maalum CHADEMA walioingizwa bungeni bila kuzingatia sheria wakaondolewa.

Sina kinyongo na kina Mdee lakini kinachoniuma ni kufinyangwa kwa sheria kiasi kwamba kama akitokea mtu akaenda kupinga jambo hili mahakamani juu ya uwapo wa wabunge hao bungeni itakuwa aibu kwa nchi maana atashinda tu kesi. Mdee mwenyewe ni mwanasheria na anafahamu fika kuwa sheria ilikiukwa kumhalalisha yeye na wenzake kuwa wabunge wa viti maalum wakati chama chao kilishawatimua.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA, MUNGU LIBARIKI BUNGE**

**Kwa maoni na ushauri tumia whatspapp namba 0762-183666 au barua pepe mwanakatwe2015@gmail.com**

## DARASA LA NDOA

# Je, uwapo wako nyumbani una mvuto na mguso kwa familia?



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka

**Pamoja na majukumu mengi ya kikazi, kazi isiwe sababu ya kudumu ya wanandoa kukosa muda wa pamoja. Dhamira ya kutengeneza muda wa pamoja ikikosekana muda hauwezi kupatikana. Kazi zisiondoe utu na thamani yetu katika familia.**

THAMANI ya mtu haipimwi kwa uwapo wake, bali kwa yale anayotenda. Je, wewe baba au mama umewahi kufanya tathmini binafsi ili kujua kama familia yako inafurahia uwapo wako au inajuta kuwa na baba au mama wa aina yako? Je, uwapo wako umeongeza au umepoteza thamani ya mwenzi wako?

Kama uwapo wako hauambatani na matendo mema kwa familia yako, unapoteza umuhimu, mvuto na mguso katika familia. Maana yake ni kwamba inawezekana umekaa katika nafasi ya mtu mwingine ambaye angeweza kuwa na mguso huo.

Jamii ina watu wa aina mbili. Kwanza, watu wenye kuongeza thamani katika maisha ya watu wengine na pili ni wanyonyaji ambao hawaongezi thamani katika maisha ya wengine. Hawa huishi kwa kutegemea thamani iliyowekwa na watu wengine.

Watu wa aina hii mara nyingi huwa ni wepesi wa kulaumu. Siku zote kinachowafanya watu wa aina hii waendelee kuwapo katika maeneo yao ya kazi ni unafiki na jitihada yao ya kufanya majungu.

Kwa maelezo haya, swali la msingi la kujiuliza kwa kila mwanandoa ni hili, je, uwapo au kutokuwapo kwako nyumbani kuna mguso au athari yoyote? Je, ukifa utakumbukwa kwa jambo lipi? Robin Sharma, mwandishi wa kitabu kiitwacho, "When you die who will cry?" anauliza swali hili zito ambalo linahitaji tafakuri ya kina.

Mwandishi huyu amekusudia kutufikirisha kwamba unapopumua haimaanishi kuwa unaishi; kwamba unapokwenda huku na kule haimaanishi kuwa unapiga hatua mbele; kwamba unapiga sana kilele haimaanishi kuwa watu wamekusikia.

Hii ina maana kuwa maisha si suala la uwapo, bali maisha hupimwa kwa mguso unaotokana na matendo mema. Swali la kujiuliza hapa ni hili, je, maisha yako yana mguso upi kwa watu wengine? Je, utakapokufa utakumbukwa kwa jambo lipi au mambo yapi?

Kimsingi, upo ili kuwabariki wengine na si kuwaumiza. Ifike mahali hata ukifa, watu wasilie kwa kuwa haupo, bali kwa sababu uliwafanyia mambo mema yaliyogusa maisha yao. Ni muhimu mtu kuwa na utambulisho mzuri kwa watu kutokana na kila jambo unalolitenda. Onyesha upekee wako kwa kutenda mema ili ukumbukwe na uendelee kuishi katika mioyo ya watu kwa kuwa thamani yako imefungamanishwa katika upekee huo.

Mume na mke ni muhimu waonyeshe upekee wao katika ndoa kwa kuwa ndoa ni wajibu. Kwa mantiki hiyo, wanandoa watambue nafasi na wajibu wao katika ndoa. Furaha na mafanikio katika ndoa vitakuwapo pale kila mwanandoa atakapotimiza wajibu wake na kumtanguliza Mungu.

Ni muhimu kila mwanandoa aitendee haki nafasi yake ya kuwa mwenzi pasipo kulazimika kuishi maisha ya watu wengine. Ni muhimu wanandoa wajifunze kuishi maisha yao ili kutunza amani na utulivu.

Ndoa si gereza. Wanandoa wanapaswa kuishi maisha yenye mguso, mvuto na kufurahiana. Hali hii haiji kimiujiza bali hutengenezwa kwa kutendeana mema ikiwa ni pamoja na kupata muda wa pamoja. Pamoja na majukumu mengi ya kikazi, kazi isiwe sababu ya kudumu ya wanandoa kukosa muda wa pamoja. Dhamira ya kutengeneza muda wa pamoja ikikosekana muda hauwezi kupatikana. Kazi zisiondoe utu na thamani yetu katika familia.

Mke au mume asiwe sababu ya kuleta upweke katika ndoa yake. Weka alama njema katika maisha ya mwenzi wako na watoto. Siku zote heshima na thamani ya mtu kwa jamii huanzia nyumbani kwake. Familia ikutambue kuwa wewe ni baba na mama unayejali na kuthamini. Onyesha upekee wako ili familia yako ikufurahie na kukuenzi. Haitamsaidia sana mtu kuonekana ni mwema sana kwa watu wengine, wakati nyumbani kwake ni mkatili.

Ni muhimu wakati wote kukumbuka kuwa, kazi inatuhitaji, lakini familia inatuhitaji pia. Kazi unayofanya ni muhimu, hali kadhalika familia uliyopewa na Mungu ni muhimu. Mke wako ni muhimu; mume wako ni muhimu na watoto wako ni muhimu. Fanya kazi kwa bidii na kutoa huduma bora kwa jamii, lakini huduma bora ianze katika familia yako.

Familia yako inahitaji sana uwapo wako. Ukiona mwenzi wako au watoto hawafurahii uwapo wako, ujue una matatizo kwani wako wazazi ambao wanaweza kuwapo nyumbani lakini wasiwapo nyumbani. Hii ina maana kuwa, baba au mama awapo au asiwapo nyumbani haleti tofauti yoyote. Uwepo wake unakosa umuhimu, mvuto na mguso katika familia. Familia haioni faida ya uwepo wa baba au mama. Tenda mema kwa familia yako ili siku zote uendelee kuishi katika mioyo yao na kubarikiwa.

Ndoa ni taasisi ambayo ni kitovu cha familia na malezi. Familia ndiyo msingi wa maadili mema kwani tabia na mienendo yetu inajengwa katika familia. Hata maadili ya viongozi yanajengwa kuanzia katika ngazi ya familia. Ili tuwe na viongozi bora na waadilifu, lazima mkazo uwekwe katika malezi ngazi ya familia. Maendeleo yanahitaji watu waadilifu. Uadilifu huo unajengwa katika familia kwanza.

Kwa maana hiyo, ndoa zikiwa imara, tutakuwa na familia imara; tukiwa na familia imara tutakuwa na jamii imara; tukiwa na jamii imara, tutakuwa na taifa imara. Maendeleo ya taifa yanategemea ndoa imara.

**Dk. Mlyuka ni Mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.**

# MAISHA

APRILI 25, 2021
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili



Ukurasa 10

**Analilia simu janja, nani alimfundisha?**



Ukurasa 15

**MAISHA NI NYUMBA**
Zulia ndani ya nyumba ni muhimu



**HARUSI**

Ukurasa 12



**ZIJALI NYWELE ZAKO**

## Kitunguu maji, tangawizi suluhisho tosha

Ukurasa 14

# Analilia simu janja, nani alimfundisha?

Na Beatrice Moses

KILIO kikali cha mtoto kinasikika, sauti ya mama anayelalamikia kilio hicho nayo inafuatia, "wewe unaniharibia simu yangu mara kwa mara hii siyo ya kuchezea tena sitaki kabisa upumbavu wako," anasema .

Pamoja na maneno hayo yule mtoto hakuacha kulia huku akijirusha rusha ovyo, kiasi kwamba angeweza hata kujijeruhi. Ninamtazama mtoto huyo ana umri wa miaka kama mitatu.

Mama yake baada ya kuona anajirusha rusha akachukua bakora na kuanza kumcharaza huku akiwa anatweta kwa hasira, bakora zilipotua mwilini wake mtoto alilia zaidi lakini akawa anaomba msamaha kuwa harudii tena.

Baada ya kusikia anaomba msamaha mama yake akamwamuru afute machozi, kisha aingie ndani haraka, vinginevyo atamcharaza viboko zaidi. Mtoto akainuka pale haraka na kuelekea ndani huku akiwa ameziba mdomo wake usitoe sauti ya kilio.



Natafakari tukio hilo kwamba japo mama kamcharaza bakora mwanaye, lakini ukweli unabaki pale pale ni yeye ndiye aliyemjengea mwanaye mazoea ya kumruhusu kuchukua simu na kuichezea kuna michezo kadhaa(game) kwenye hizo simu janja.

Ni wakina mama wengi wamekuwa na tabia hiyo kutokana na upendo kwa watoto wao kuamua kuwakabidhi simu zao za mkononi na kuwaruhusu kucheza michezo ya simu.

Bila kujali gharama za simu janja hizo ambazo inawezekana bei ya chini inaanzia 150,000 zipo hadi za milioni kadhaa , kulingana na ubora na jina la kampuni iliyotengezeza.

Licha ya kwamba kuna vifaa maalum vya kuchezea watoto ikiwamo wanasesere ni miongoni mwa vitu ambavyo baadhi ya wazazi wamekuwa wakitilia maanani kuvinunua, zipo pia hizo michezo maalum kwa ajili yao.

Japo sababu za kiteknolojia zimesababisha mabadiliko ya kitabia na uelewa wa watoto , bado kuna vifaa vyao pia ambavyo vimetengenezwa kwa kuzingatia teknolojia hiyo mpya ambavyo vina manufaa kwao kuliko simu ya mkononi.

Kwani licha ya kuwa matumizi ya simu hizo yanahusiana na mionzi ambayo inatajwa siyo salama hasa kwa watoto, hivyo kumnyima simu ya mkononi mtoto ni jambo sahihi na linalomhakikishia usalama wake.

Wakina mama kadhaa wamejikuta kwenye wakati mgumu ikiwamo kuharibiwa kwa vifaa hivyo na watoto, pia wanakosa mawasiliano kwa muda kadhaa na kulazimika kutafuta fedha za kununua ama kufanyia matengenezo simu zao.

Ukweli wa mambo ni kwamba ni vyema wazazi kutambua kuwa kifaa hizo siyo kwa ajili ya kuchezea watoto bali hicho ni kwa matumizi ya mtu mzima ambaye anajitambua. Ndiyo sababu hata baadhi ya hizo gemu ukizifuatilia vyema hazimjengi mtoto kifikra bali zinamharibu kwa kuwa siyo kwa ajili yake.

Kutumia simu ya mkononi kama mwanasesere kubembelezea mtoto siyo jambo sahihi, unaogopa mtoto asilie kwa kumnyima hiyo simu lakini unahatarisha maisha yake.

## NA HAMIS KIDAGO 0657 207168 QUIZ

**Weka maneno yafuatayo katika mtitiriko utakaoyafanya yalete maana kamili.**

**Les articles partitifs**

Angalia kwa makini mfano huu wa "articles partitifs" katika maelezo yafuatayo, kasha ujibu maswali yatakayofuata kuhusu hizo "articles partitifs".

**N.B. (ms) nimasculinsingulier, (fs) niféminsingulier.**

.Cestgentil à toi de faire les courses: alors, s'ilteplaît, tuachetesdu riz (ms), del'eau (fs), de laviande (fs) et de l'huile (fs) et tuprendsde l'argent (ms) dansmon sac.

Malizia maneno yafuatayo kwa kutumia "articles partitifs" zinazoendana.

Du poivre (ms)

.........jambon (ms)

.........huile (fs)

..........parfum (ms)

............fromage (ms)

............crème fraîche (fs)

............pâté (ms)

...........bière (fs)

............vinaigre (ms)

...........rouge (ms) à lèvre

..............saucisse (fs)

...............sucre (ms)

..............eau de toilette (fs)


..............beurre (ms)

**Chagua jibu sahihi katika mabano kukamilisha sentensi zifuatazo.**

Le matin, je prends (du – de l') café (ms) ou (du – de l') thé (ms) et les enfantsprennent (de la - du) lait (ms) chaud. À midi, à la cantine, je choisissouvent (de la – de l') salade (fs) ou (de la – de l') omelette (fs). Le soir, je prépare (de la – du) soupe (fs), surtoutl'hiver. Nous mangeonssouvent (du – de la) viande (fs) froideou (du – de l') poisson (ms).

## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA



Alichokifanya Adaktari

MFUGAJI mmoja alikwenda kwa mfugaji mwenzake akitaka msaada, lakini alipofika alimkuta mtoto peke yake.

**Mkulima:** Baba yako yupo?

**Mtoto:** Hapana Mzee, amekwenda mjini.

**Mkulima:** Mama yako?

**Mtoto:** Nae kaenda mjini na baba.

**Mkulima:** Kaka yako yupo?

**Mtoto:** Nae hayupo, wote wamekwenda mjini.

Kwani una shida gani? Kama una shida ya kuangalia mifugo wacha nikavae koti twende nikakusaidie.

**SWALI**

Zao la karafuu linalimwa wapi visiwani Zanzibar?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Waliofanikiwa katika ndoa walipambana na matatizo

KARIBU tena msomaji wangu katika safu yetu ya Maisha Ndivyo Yalivyo. Bado tunaendelea na vita vya maisha tunayokumbana nayo kila uchao. Leo nigeukie anga la ndoa na mwarobani wa kuleta mabadiliko katika yale wanandoa wengi wanapitia katika maisha.

Eneo la ndoa si la kupuuzia. Ni lazima watu wakae chini na kuanza kuchambua ni kwa nini ndoa nyingi hazina amani, upendo, utulivu, uaminifu na kadhalika. Ukweli ni kwamba tunahitaji msaada mkubwa sana wa ki-ungu.

Pale tunapogundua chanzo cha matatizo ya ndoa, nina uhakika tutapata msaada kutoka juu, utakaobadilisha maisha ya wanandoa wengi. Katika eneo hili, tunahitaji hekima ya Mungu maana hekima ya kibinadamu haiwezi kutatua matatizo haya.

Kwa mantiki hiyo, tatizo kubwa ambalo mtu anaweza kuwa nalo ni kushindwa kupata msaada kutoka kwa Mungu. Suluhu la matatizo ya ndoa huanza pale tu mtu anapomruhusu Mungu kuingilia kati kwani hakuna linalomshinda.

Huenda umeteseka kwa muda mrefu, huenda umeshakata tamaa kuhusu ndoa yako na labda umeapa kuwa hutakaa ujihusishe na mambo yoyote yanayohusu ndoa. Tafuta kwa bidii nguvu ya Mungu kwani yeye ni muweza wa yote.

Watu wengi ambao wamekuwa na mafanikio katika ndoa zao haikuwa rahisi kama tunavyodhani. Walianza na matatizo makubwa sana ambayo hawakuwahi kutarajia.

Pengine walikataliwa na wakwe, mawifi, walidharauliwa na wenzi wao.

Hata hivyo, wenye matatizo makubwa kwenye ndoa, wana uwezo mkubwa wa kuleta mabadiliko kwenye ndoa hizo. Tatizo ni kwamba wanadharau huo uwezo ulio ndani yao.

Hivyo, wengi wamejikuta wakikata tamaa, ilihali walitakiwa kuongeza bidii kidogo ya kuita neema na nguvu ishuke juu ya ndoa zao. Kama uko tayari kupata msaada wa kiungu, matatizo ya ndoa uliyo nayo yatakuwa ni historia. Mungu atabadilisha matatizo yako kuwa miujiza na ushuhuda wako kuwatia nguvu maelfu ya wengine.

Inahuzunisha kwamba wengi wamepoteza mwelekeo katika eneo hili la ndoa. Wako baadhi walikuwa wanatarajia kupasua katika ndoa, lakini ndio kwanza wanapambana. Wengi wamepoteza fedha, fursa na wadhifa kwa sababu ya masuala ya ndoa.

Wengine wamechanganyikiwa maana wanakumbana na maadui zao kila kona.

Wanashambulia biashara zao, familia zao na hata jamii zao. Inawezekana kabisa unahisi umezungukwa na maadui. Hakuna sababu ya kuogopa. Jambo la msingi ni kufahamu kuwa Mungu ana kitu kwa ajili ya ndoa yako.

Watu wengi sana leo wamechanganyikiwa hawajielewi kabisa. Mara zote hujiuliza maswali kama, “Je, mimi nina tatizo gani?, ni kitu gani kinaendelea kwenye maisha yangu? Mbona namcha Mungu lakini bado nateseka? Mbona sioni mafanikio yoyote, kwanini ndoa yangu haijatulia?

Ni ukweli usiopingika kwamba ndoa ni moja ya matatizo makubwa mwanadamu anaweza kupitia katika maisha. Ni rahisi kukabiliana na changamoto za biashara lakini siyo mafarakano katika ndoa.

Kadhalika nimekuja kugundua kuwa matatizo makubwa katika ndoa za watu wengi yana chimbuko refu sana la kishetani.

Wengi wenye misukosuko katika ndoa hawajui kuwa nguvu za giza zimeachiliwa kuua hatma za maisha yao.

Nguvu za giza zinashambulia ndoa zao kama njia mojawapo ya kuua hatma zao. Wapo mawakala (wanadamu) wa shetani wameachiliwa kufuatilia mtu yoyote anayelalamika ana mafarakano katika ndoa ili wamuangamize kabisa.

Kuna baadhi ya ndoa ambazo shetani huzichukia kwa kiwango kikubwa kwa kuwa zinaharibu ufalme wake. Hivyo hufanya juu chini ili ndoa hizo zisitokee. Shetani na mawakala wake wamelenga kuangamiza hivyo ni lazima upambane katika vita hiyo na ushinde. Mwenye nguvu atamshinda aliye dhaifu.

Wako wanaopambana na vitu usiku, wanaota ndoto wakiwa na watu wasiowafahamu. Wanaona ni jambo la kawaida kumbe shetani kamtafutia mume au mke wa kwenye ndoto.

Wanandoa wanaokumbana na mazingira hayo, ndoa zao hazitulii kumbe yupo adui asiyejulikana amejificha.

Mpenzi msomaji, ndoa ni moja ya misingi ya uumbaji wa Mungu. Ndoa siyo bahati mbaya. Ukiingia kwenye ndoa unatakiwa kukaa, ukioa mmoja anaondoka lipo tatizo.

***Wiki ijayo nitaenda zaidi kuchimbua kwa nini mashauri mengi ya ndoa yametinga mahakamani kwa talaka. Je, una maoni, kisa cha maisha? Tuma ujumbe kupitia 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Rais Samia kashasema, unatakiwa utekelezaji

HOTUBA ya mwelekeo wa serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, imegusa maeneo yote muhimu ambayo kukiwa na usimamizi na utekelezaji madhubuti kutainufaisha Tanzania na Watanzania.

Kila sekta imeguswa kwa namna ambavyo itachangia katika ukuaji wa uchumi wa nchi ili kuendelea kushikilia nafasi ya uchumi wa kati wa kipato cha chini na hata kufikia uchumi wa kati.

Watanzania, nikiwamo, wana matarajio makubwa kwa viongozi ambao wamepewa dhamana ya kuwaongoza, ikiwamo kuwawakilisha ipasavyo katika ngazi mbalimbali.

Rais alilitaka Bunge ambalo ni kusanyiko la uwakilishi wa wananchi kutoka kwenye majimbo na kada mbalimbali, ambalo pale ndipo sauti zinapaswa kusikika zikieleza matatizo ya wananchi bila kujali itikadi zao, liikosoe serikali.

Bunge lina wajibu wa kuisimamia serikali ipasavyo pia kuishauri, ndiyo maana Rais ametoa nafasi ya kukosolewa tena akasisitiza kukosolewa vikali ili kuiwezesha serikali kutekeleza wajibu wake ipasavyo.

Kwa kauli hii maana yake tutaona bunge linajikita katika agenda muhimu ambazo zinagusa maisha ya wananchi moja kwa moja, kuliko agenda binafsi. Sasa serikali itatoa majibu sahihi kwa mambo ya msingi ambayo wakati mwingine hayajapata ufumbuzi.

Ninaamini kama bunge litasimama katika nafasi yake. Maana yake tutakuwa na mhimili imara utakaosimamia vyema serikali kwa mujibu wa Katiba na ajenda za wananchi zitawasilishwa vyema na mwamko wa kupiga kura utaongezeka.

Hakuna ubishi kuwa wabunge ni kundi linalolipwa vizuri kuanzia posho, mshahara na kiinua mgongo ambacho hakikatwi kodi. Lakini pia mbunge ana nafasi ya mikopo mikubwa huku kukiwa na fedha za mfuko wa jimbo.

Haitarajiwi kwa huduma hizi bado atashidwa kutimiza wajibu wake kwamba yuko ambaye tangu ameingia bungeni hajawahi kuuliza swali, kutoa mchango wake badala yake alishia kupiga kofi.

Kwa sasa makadirio ya mapato na matumizi kwa wizara mbalimbali yanawasilishwa na wabunge wanatoa michango yao na mwisho itakuja bajeti ya serikali ambayo itaonyesha vyanzo vya mapato na namna keki ya taifa itakwenda kugawanywa.

Uwakilishi wa wananchi uonekane na kweli sauti zao zisikike kupitia wawakilishi wao. Tusikie wabunge wakiibua matatizo ya maji, miundombinu, pembejeo, afya, elimu na mengine mengi yanayohitaji kusemewa katika maeneo mbalimbali.

> **“Kwa kuwa ili afanikishe hayo ni lazima kuunga mkono kuanzia kwa mwananchi wa kawaida kabisa hadi wa ngazi ya juu.**

Aidha, Rais aligusia suala la wizi na ubadhilifu wa mali ya umma ambao umeanza kujitokeza katika baadhi ya mashirika ya umma, na kuahidi kuwa mkali ili kuhakikisha fedha za Watanzania zinakuwa salama na zinafanya mambo ya msingi.

Pamoja na wabunge kutimiza wao, nasi Watanzania tunapaswa kumuunga mkono Rais kwa kufanya kazi kwa bidii katika maeneo yetu na hasa tukizingatia kuwa sasa anakwenda kuimarisha sekta binafsi ambayo ndiyo injini ya uchumi wa nchi.

Iwapo hotuba hiyo itazingatiwa kipengele hadi kipengele, naamini baada ya miaka mitano kutakuwa na tiki nyingi katika yaliyotekelezwa huku machache sana yakibaki kwa sababu mbalimbali ikiwamo ya kibajeti.

Rais ameshasema amemaliza, kazi kwetu kutekeleza, kwa kuwa ili afanikishe hayo ni lazima kuunga mkono kuanzia kwa mwananchi wa kawaida kabisa hadi wa ngazi ya juu.

# HARUSI







Ilikuwa shamrashamra wakati Zuwena Hussein Poyo alipoamua kukubali kufunga ndoa na Ahmed Yusuf Ahmed na kuwa mume wake. Harusi hiyo ilifungwa Aprili 9, mwaka huu jijini Dar es Salaam. (Kama unapenda harusi yako ionekane katika ukurasa huu wasiliana nasi kwa namba: 0717336368 au barua pepe: Moshilusonzo@gmail.com)





# MITINDO







## VAZI LA SARI

# Kutoka India hadi Tanzania

SARI ni jina la nguo maalum zinazotumiwa na wanawake wa jamii ya Kihindi wakati wa harusi.

Kwa ujumla nguo ya Sari inaheshimika na kuonekana ya kipekee kutokana na umuhimu wake katika jamii hiyo.

Hata hivyo, kutokana na utandawazi jamii nyingi wakiwamo Waafrika, wamekuwa wakitumia vazi hilo katika shughuli mbalimbali za kijamii.

Kipimo halisi cha Sari, ni lazima kitambaa kiwe na ukubwa wa 4 hadi 9.

Vitambaa vya Sari hutengenezwa kwa hariri, velvet na pamba. Kitambaa cha Sari kinatengenezwa kwa kutumia vifaa vya kiasili na ubora wake unakuwa wa hali ya juu.

Nguo ya Sari kawaida hujazwa na mapambo ili kitambaa kionekane kinang'ara.

Wabunifu wamebuni mitindo tofauti ya vazi la sari na kutumiwa na watu wa aina mbalimbali ikiwamo Watanzania ambao wanataka kuonekana tofauti katika harusi zao.

Baadhi wanapenda kutengenezewa Sari katika mitindo ya kisasa, ikiwamo kushonewa sketi na blauzi yenye mkono mmoja.

Wanawake wenye maumbo tofauti wanaweza kuvaa mtindo wa nguo hizi za nguo za Sari.

UREMBO



ZIJALI NYWELE ZAKO

# Kitunguu maji, tangawizi suluhisho tosha

NYWELE nyepesi na zinazokatika huwa zinaleta mfadhaiko kwa mwanamke anayependa urembo.

Hata hivyo, tatizo hilo limekuwa sugu baadhi ya watu haswa wanawake. Katika kutatua tatizo watu wanapoteza pesa nyingi wakihangaika kutafuta matibabu, lakini hawafanikiwi.

Kutokana na tatizo hilo kuwa kubwa, nitakupa njia rahisi ya kupambana na tatito hili kwa kutumia tangawizi na kitunguu maji.

Tangawizi na kitunguu pamoja na kuwa ni kiungo muhimu kwenye chakula, lakini ikitumika kama tiba inaleta matokeo mazuri.

Kutokana na Tangawizi kuwa na utajiri wa madini ya magnesium, potasium , phospate pamoja na vitamini mbalimbali inasaidia kuboresha afya ya nywele na hivyo kuzuia kukatika.

Kitunguu maji pia kinasaidia kupambana na bacteria wanaoweza kusababisha magonywa ya ngozi ya kichwa kama mba ambao huchangia kukatika kwa nywele.

Ili kutumia viungo hivi kama tiba ya nywele unatakiwa kusaga tangawizi pamoja na kitunguu maji, kisha kuchuja na kupaka mchanganyiko huu kichwani.

Tumia kofia ya plastiki kufunika nywele zako kwa dakika 15 na baada ya hapo osha kwa maji baridi na shampuu.







MAPISHI

Na Mary Geofrey



# Futari ya tambi za mayai

LEO katika safu yetu ya mapishi tutaelekezana namna ya kupika futari ya tambi za mayai.

**MAHITAJI**

Tambi nusu paketi, vitunguu maji viwili vikubwa, karoti moja, hoho moja na vitunguu swaumu vilivyokatwa vipande vidogo kijiko kimoja cha chakula.

Mahitaji mengine ni carry powder kijiko kimoja cha chai, njegere zilizochemshwa nusu kikombe, mafuta kwa kiasi upendacho, mayai mawili na chumvi kwa ladha upendayo.

**NAMNA YA KUPIKA**

Chemsha maji ya moto yanayotokota, ongeza chumvi na mafuta kidogo, weka tambi kwenye maji hayo chemsha hadi ziive.







Baada ya kuiva epua na chuja maji yote ili kupata tambi kavu.

Ziweke kwenye bakuli piga mayai kisha weka pembeni.

Chukua kikaango na weka mafuta, vitunguu maji, vitunguu swaumu, pilipili, hoho, karoti na carry powder Kisha kaanga kwa pamoja katika moto mdogo kwa muda mfupi kwani mboga hazitakiwi kuiva.

Ongeza tambi na njegere katika kikaango, geuza kila mara ili kuchanganya. Weka mayai kwenye tambi kisha geuza kwa haraka bila kupumzika adi mayai yaive na tambi ziwe kavu na zitakuwa tayari kwa kuliwa.

Ukitaka tambi zako zisivurugwe yaani ziwe kavu kama chips yai, ukiongeza mayai usizigeuze hadi unapoona yai limeiva kwa chini unageuza upande wa pili.

Furahia futari yako kunywa na uji wa ulezi, juisi, soda au chai.

MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Zulia ndani ya nyumba ni muhimu

ZULIA ndani ya nyumba ni muhimu sana katika kuongeza mvuto. Japokuwa si la lazima sana, linapowekwa huongeza thamani ya nyumba.

Ikumbukwe kuwa kuna aina mbalimbali za zulia. Liko kubwa la kutandika sebule nzima, la kutumika kutandika sehemu ya kuweka samani pekee, dogo kiasi la kutumia katikati ya meza na dogo kabisa la kutumika mlangoni, koridoni au bafuni kwa ajili ya kufutia miguu.

Leo nazungumzia zulia linalotandikwa kuendana na mpangilio wa samani za ndani.

Mara nyingi tunapolitandika kwenye nyumba zetu, huwa tunakosea vitu vidogo, lakini leo tunataka tuangalie namna bora tunapoamua kulitandika.

Ni vyema kabla ya kulitandika, ukahakikisha umelipima kulingana na ukubwa wa eneo zinapopangwa samani ili usiende tofauti na lengo na kuhakikisha miguu ya samani inakuwa ndani ya zulia.

Jambo lingine ni kuhakikisha unachagua zulia linaloendana na baadhi ya rangi za mapambo mengine ya sebule yako. Kwa mfano, endapo chumba kina muundo wa duara, ni vyema pia zulia litakalotumika kutandikwa liwe na umbo la namna hiyo.

Ni vizuri kuepuka kuweka zulia tofauti na hilo kwa sababu linaweza lisienee au likakosa utulivu au ukalilazimisha kutokana na kutolipima kabla, hivyo likaonekana kama limetuna ovyo.

Kwa chumba chenye pembe nne, nacho kitahitaji kuwa na zulia la muundo huo. Endapo chumba ni kirefu zaidi na chembamba, nunua zulia la kukata kwa kuzingatia mpangilio mzuri wenye vipimo kulingana na namna unavyopanga kuweka eneo lako.

Endapo umeweka zulia la kuenea sebule yote na ni la rangi moja, ni vizuri ukatupia zulia ndogo kwa juu ili kuleta mvuto zaidi.

Aidha, epuka kufananisha rangi ya zulia na kila kitu kilichopo katika chumba chako. Tambua kwamba ukichanganya rangi mbili au tatu ndani ya chumba hazichoshi sana na unaweza kupata mwanya mkubwa wa kupendezesha na kufanya mabadiliko ya baadhi ya vitu hususani pazia na urembo mwingine.

Kumbuka kuwa hata usipoweka zulia ndani ya nyumba au sebule, hakuna kinachoharibika.





## Dondoo namna ya kupangilia 'dressing table' chumbani kwako

**1:** Kwanza unatakiwa kujua droo za dressing table sio za kuwekea madaftari wala vitu vingine, bali maalum kwa ajili ya vipodozi.


**2:** Kama dressing table yako haina droo, jaribu kupanga vitu kwa mpangilio mzuri juu ili kuhakikisha vitu havizagai ovyo.

**3:** Kama ni vitu vingi katika meza yako ya urembo, hakikisha unatumia mabegi maalum ya kuhifadhia vipodozi kuweka baadhi ya vitu.

**4:** Unatakiwa kuwa mbunifu kwa kuangalia dressing table za marafiki zako, ili kupata mwonekano mzuri na matumizi sahihi ndani ya chumba chako.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2021
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
KIMBUNGA 'SHOBO' KWANI KIMESHATUA KWETU?
SIO SHOBO NI JOBO... KINGEKUWA SHOBO TUNGEKISHOBOKEA..
MHISHIMIWA AHADI NI DENI NAONA SIKU ZINAYOYOMA USOMEKI!
WEEEE!!! USINITAFUTIE JANGA, MAMBO YA FALAGHA HAYAHUSIANI NA SIASA.
UNAJUA WIVU UNAONIFANYIA UNAZOROTESHA MAENDELEO?
'YAZOROTE' LAKINI HUTOKI KWENDA BAR.
TUMEZOEA MAMBO SIRIAZI KUYAFANYIA MZAHA MITANDAONI!
WE TAZAMA HIKI KIMBUNGA, TAYARI WAJUAJI WANAZUA YAO!
WAMEKUWA WASEMAJI KABLA YA WASEMAJI!
NI SHIDA!
WEWE HUSIKII...
POTELEA MBALI... DALALI GANI HUNA UMAARUFU!
TWENDE WAPI WE BABU! UNATAKA TUZOLEWE?
KIMBUNGA KIME-SHANIHARIBIA "TAIMING"
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...KWA MOLA NI MADOGO

## HABARI KIMATAIFA

# Umoja wa Mataifa waionya Somalia

**New York,** MAREKANI

BARAZA la Usalama la Umoja wa Mataifa, limepitisha tamko la kuwataka viongozi wa vyama vya siasa nchini Somalia kuacha kuvutana na badala yake kufanya mazungumzo ili kuondoa mkwamo wa uchaguzi

Baraza hilo lilipitisha azimio hilo, siku ya Ijumaa na kuvitaka vyama hivyo kuacha vurugu na kurudi kwenye meza ya mazungumzo bila kuweka masharti kama njia ya dharura.

Hatua hiyo ilichukuliwa kama kuonyesha msisitizo juu ya wasiwasi wake kuhusu mgogoro wa kisiasa wa nchi hiyo ya pembe ya Afrika.

Waraka wa tamko hilo umefafanua kwamba wanachama wa baraza la usalama wameelezea wasiwasi wao kuhusu mkwamo wa kisiasa unaoendelea na mivutano miongoni mwa viongozi wa kisiasa nchini humo kuhusu kuitishwa kwa uchaguzi mkuu.

Mnamo Machi mwaka huu, baraza hilo la usalama liliwataka viongozi wa serikali ya Somalia kutatua mvutano uliopo juu ya mchakato wa uchaguzi. Hata hivyo ilishindikana wakati Rais Mohammed Abdullahi Farmajo yakionekana kikwazo baada ya kujiongezea muda wa kukaa madarakani wa miaka miwili.

Hata hivyo bunge la nchi hiyo, lilipitisha muswaada wa sheria mwanzoni mwa mwezi huu uliomuongezea rais muda wa kubakia madarakani kwa kipindi cha miaka miwili, lakini haukufikishwa katika baraza la Seneti.

Kutokana na hali hiyo, vyama vya upinzani vilikosoa hatua hiyo wakisema umekwenda kinyume na katiba ya nchi.

Rais wa Somalia na viongozi wakuu wa majimbo matano yenye mamlaka yao ya ndani katika shirikisho la Somalia, walikuwa na makubaliano yaliyofikiwa mwezi Septemba mwaka jana yaliyofungua njia ya kufanyika uchaguzi wa bunge na rais usiokuwa wa moja kwa moja uliotakiwa kufanyika mwishoni mwa 2020 au mwanzoni mwa 2021.

Lakini viongozi hao waliingia kwenye mvutano wakitofautiana kuhusu namna uchaguzi huo utakavyofanyika na duru kadhaa za mazungumzo ya kujaribu kuondoa mkwamo huo zikishindikana.

Sheria mpya nchini humo inafungua njia ya kufanyika kwa mara ya kwanza uchaguzi utakaomhusisha moja kwa moja kila mpiga kura wa nchi hiyo kumchagua kiongozi anayemtaka.

Uchaguzi wa namna hiyo haujawahi kufanyika nchini Somalia tangu mwaka 1969 na wasomali wamekuwa wakipewa ahadi hiyo kwa miaka kadhaa na hakuna serikali.

Tamko hilo la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa limebaini kwamba mkwamo wa kisiasa nchini humo pia umesababisha kutofuatiliwa kwa masuala muhimu yanayoipa changamoto nchi hiyo kama vile mafuriko, ukame, uvamizi wa nzige, janga la Covid-19 pamoja na vita dhidi ya kundi la wanamgambo wa itikadi kali la al-Shaaba.

**DW**




Nyambizi ya Indonesia ambayo imepotea baharini kwa muda wa siku nne, jeshi la nchi hiyo lina hofu askari wake 53 wanaweza kupoteza maisha kwa kuishiwa hewa ya Oksijeni. **(PICHA: AFP)**

# Israel, Palestina hofu yatanda

**Tel Aviv,** ISRAEL

HALI ya wasiwasi imetanda katika mpaka wa Israel na Gaza baada ya kuwapo madai ya wanamgambo wa Palestina kurusha roketi 36 usiku wa kuamkia jana.

Jeshi hilo la Israel, lilisema mfumo wa kuzuia makombora wa Israel ulizuia roketi sita na nyingine hazikufika kwenye eneo la Israel.

Kulingana na taarifa hiyo, Israel ilijibu hatua hiyo kwa kushambulia maeneo ya kijeshi ya Gaza ambayo ni pamoja na miundombinu ya chini ya ardhi na vifaa vya kufyatulia roketi. Maofisa wa usalama wa Hamas pamoja na mashuhuda waliliambia shirika la habari la DPA, kwamba kulikuwapo na uharibifu wa mali katika maeneo yaliyolengwa katika eneo lote la Ukanda wa Gaza.

Hakukuwa na taarifa yoyote ya majeruhi kutoka pande zote.

**DW**

## Marekani kutambua mauaji yaliyotokea 1915 kuwa kimbari

**Washingyon,** MAREKANI

RAIS wa Marekani, Joe Biden, anakusudia kuyatambua mauaji ya Waarmenia ya mwaka 1915 katika Dola ya Ottoman kama mauaji ya Kimbari.

Biden alimueleza Rais wa Uturuki, Tayyip Erdogan, kusudio lake hilo wakati walipofanya mazungumzo ya kwanza kwa njia ya simu ikiwa ni miezi mitatu tangu aapishwe kuwa kiongozi wa taifa hilo.

Ikulu ya Marekani maarufu kama White House, ilidai kuwa Biden analenga kuimarisha uhusiano baina ya nchi hizo mbili ikiwa ni pamoja na kufanya mkutano wa pande mbili wakati wa mkutano wa kilele wa Jumuiya ya kujihami NATO utakaofanyika mwezi juni mjini Brussels nchini Ubelgiji.

Mazungumzo ya viongozi hao wawili yalifanyika siku moja kabla ya kumbukumbu ya mauaji ya Waarmenia siku ya jana.

**DW.**

## Vifaa kutoka nyambizi iliyopotea vyapatikana

**Jakarta,** INDONESIA

MKUU wa jeshi la Indonesia, amesema vikosi vya uokozi vimefanikiwa kupata baadhi ya vifaa vilivyokuwapo kwenye nyambizi iliyopotea katika kisiwa cha Bali.

Ofisa wa ngazi za juu wa jeshi la anga, Hadi Tjahjanto, alisema vifaa vilivyopatikana ni pamoja na chupa ya mafuta ya vilainishi pamoja na kifaa kinachozuia makombora.

Alisema wana imani kwamba vifaa hivyo vilivyopatikana kwenye eneo ambako nyambizi hiyo ilionekana mara ya mwisho kuwa ni sehemu ya meli hiyo.

Tjahjanto, alisema vifaa hivyo visingeweza kutoka vyenyewe isipokuwa tu inapotokea vinalazimizishwa kutoka.

Nyambizi hiyo ilipotea ikiwa na wafanyakazi 53, na awali ilielezwa watu hao wangeishiwa na gesi ya Oksijeni mapema jana.

**DW**

## MAKALA

# TRA MKIYAFANYA HAYA KODI ZITALIPWA VIZURI



Na Magabilo Masambu

**Wakishavaa kawaida wanazunguka kwenye biashara za watu kujionea jinsi wanavyofanya biashara kupiga nao stori, kisha kujitambulisha kwao na kwamba tumekuja angalau kubadilishana nanyi mawazo tuone mnakwama wapi.**

BASI utuambie, waonaje? Ni halali kumpa Kaisari kodi ama sivyo? Lakini Yesu akaufahamu uovu wao, akasema mbona mnanijaribu enyi wanafiki? Nionyesheni fedha ya kodi. Nao wakamletea dinari, akawaambia ni ya nani sanamu hii na anwani hii? Wakamwambia ni ya Kaisari. Akawaambia basi mlipeni Kaisari yaliyo ya Kaisari na Mungu yaliyo ya Mungu. Waliposikia walistaajabu wakamwacha wakaenda zao.” (Mathayo 22:17-22)

Ukweli ni kwamba masuala ya kodi hayakuanza leo bali miongo mingi iliyopita. Maandiko yanaonyesha kwamba anayestahili kulipwa kodi basi alipwe na anayestahili sadaka pia apewe sadaka yake. Maana yake, kodi ya haki ndiyo inayotakiwa kulipwa, si kubambika kodi isiyostahili ili mtu ashindwe kulipa mazungumzo ya rushwa yaanze.

Sheria inampa uhalali mkusanya kodi wa Tanzania kufanya hivyo lakini mazingira, hekima na busara, vinatoa nafasi ya namna bora ya kuitumia Sheria hiyo ili kupata fedha za kodi bila kutumia nguvu.

Bahati mbaya, wakusanya kodi wetu wamekuwa wakidhani kwamba njia za nguvu zinazotumika katika kuidai hiyo kodi ni sahihi.

Ni muhimu serikali itambue kwamba walipakodi ni wateja wao si maadui kama ambavyo tumekuwa tukishuhudia kodi zinadaiwa kwa kutumia vikosi vya polisi. Hawa watu wanahangaika peke yao kutafuta mitaji, sasa kwa nini kwenye kukusanya kodi iwe kama mmechangia mtaji, pamoja na kwamba Sheria inalazimisha kulipa kodi. Sheria hailazimishi kufanya biashara, hivyo mtu akiona ni kero anaweza kubadili kazi asifanye biashara. Kudai kodi ni lazima itumike akili yenye kutia hamasa ili watu walipe kodi huku wakiwa na furaha.

Serikali inatakiwa kuwa mlezi, hivyo isiwe na jukumu moja tu la kudai. Maofisa wa kodi wasiwe kazi yao kukaa tu ofisini na kwamba siku wakijisikia kudai kodi ndipo wanatoka kwenda mtaani, kumbe kinachotakiwa wakati mwingine wanaweza kuvaa kawaida kama raia wengine bila zile tai zao ambazo watu wameshakariri kwamba ukiwaona basi ujuwe ni kodi. Wakishavaa kawaida wanazunguka kwenye biashara za watu kujionea jinsi wanavyofanya biashara kupiga nao stori, kisha kujitambulisha kwao na kwamba tumekuja angalau kubadilishana nanyi mawazo tuone mnakwama wapi.

Yafuatayo yakifanyika yatasaidia sana watu kulipa kodi. Moja, kila meneja wa TRA mkoa anatakiwa kuwa na orodha ya wafanyabiashara wakubwa ndani ya mkoa. Ukisha kuwa na orodha hiyo, basi mara kwa mara unakutana nao kujadili changamoto wanazokumbana nazo katika ufanyaji wa biashara zao. Vikao hivyo vitawasaidia wafanyabiashara hao kueleza wapi wanahitaji masaada wa serikali ili kufanya biashara zaidi na kuwezesha kupata fedha na kulipa kodi zaidi.

Simaanishi wafanyabiashara wa kati au wadogo kwamba hawana maana bali naamini changamoto za kibiashara za hawa wakubwa zikishatatuliwa basi hawa wa chini pia watakuwa na uwezo wa kufanya biashara zaidi na kwa wingi.

TRA kupitia vikao wasijikite kuwa wanatoa elimu ya mlipakodi pekee. Waende mbali zaidi na kutoa elimu ya namna bora ya kufanya biashara kwa kuwa wafanyabiashara wengi hawana elimu ya biashara japo wanafanya biashara. Ikiwezekana pia wawaunganishe na masoko ili bidhaa zipatikane na kuuzika kwa urahisi. Vikao hivyo viwe vya mara kwa mara ili kujenga uhusiano mzuri baina ya TRA na wafanyabiashara hao.

Pili, ni muhimu kuanzisha mashindano ya walipakodi wazuri na waaminifu ndani ya mkoa. Hili litamfanya kila mtu apambane ili kuwa mlipakodi bora ndani ya mkoa. Mashindano hayo yaambatane na zawadi za washindi kwa kufanya hivyo watu wengi watajikuta wanalipa kodi vizuri.

Siku ya kukabidhiwa zawadi iambatane na hafla ikiwezekana na chakula cha pamoja, kujenga uhusiano zaidi na maofisa wa kodi, washindi watangazwe na kutambuliwa kwa vyeti safi pamoja na zawadi zao, maana yake hata viongozi wa wafanyabiashara watatokana na washindi hawa. Ushindi huo uwe katika madaraja la kwanza, pili na tatu ili hawa wa chini wawe wanapambana kuwazidi wa juu.

Tatu, matumizi ya kodi zetu. Ukishaanzisha mambo mbalimbali ambayo yatawafanya wafanyabiashara walipe vizuri kodi, kinachofuatia ni matumizi mazuri ya kodi zao, yaonekane kwenye huduma za jamii kama afya, elimu na miundombinu badala ya kusikia kwamba kodi za Watanzania zinatafunwa na baadhi ya viongozi ambao si waaminifu serikalini. Hata ikisikika hivyo, basi lazima hatua kali za waziwazi zichukuliwe ili kujenga imani kwa walipakodi kwamba kodi yao inatumika vyema.

Mataifa mengine wanalipa vizuri kwa sababu wana imani kodi zinafika na zinafanya kazi zao za kijamii. Sisemi kwamba huko hakuna wakwepa kodi bali wengi wana imani kubwa juu ya matumizi ya fedha zao.

Hapa si mara moja unasikia mlipakodi anasema “kodi zenyewe wanakula tu” kwa hiyo kwa kweli serikali lazima irudishe imani hiyo kwa walipakodi kwa vitendo badala ya maneno matupu.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Msuko ya ‘twende kilioni’ ulivyotikisa



Na Adam Fungamwango

**Wanawake walikuwa wakisukana bure kabisa. Labda ni kwa sababu wakati huo bado Watanzania walikuwa wanaishi kijamaa. Sikuwahi kuona hata siku moja mwanamke akimsuka mwenzake akalipwa kama ilivyo hivi sasa.**

UKIPITA sehemu mbalimbali nchini, mijini na vijijini, siku hizi kuna saluni za kike na za kiume. Kusambaa kwa umeme sehemu nyingi za nchi, kumesababisha kuwapo kwa saluni nyingi. Hii pia imesababisha ajira kwa baadhi ya vijana.

Zamani, mpaka katikati ya miaka ya 1990, hata kwenye jiji kubwa kama la Dar es Salaam usingeweza kukuta umeme kwenye nyumba nyingi. Nyumba zilizokuwa na umeme zilihesabika. Labda kwenye nyumba ambazo zilikuwa na maduka. Hata baadhi yao ziliweka taa aina ya karabai ambazo zilikuwa zinawaka mithili ya taa za umeme. Kwa sasa karabai si nyingi sana.

Mikoani na vijijini ndiyo kabisa. Umeme ilikuwa hadithi ya kufikirika. Mpaka mjini, tena kwenye majengo machache ya serikali.

Kutokana kutosambaa sana kwa umeme miaka ya nyuma, watoto wengi, vijana na hawa watu wazima walikuwa wanakwenda kunyoa nywele zao sehemu fulani ambazo zilikuwa maarufu sana wakati huo.

Ni chini ya mti. Saluni zilikuwa chini ya miti mikubwa. Waliokuwa wananyoa wengi wao walikuwa watu wazima kwa umri. Walikuwa wanatumia mikasi na wembe. Hakukuwa na ulazima ya mti fulani utumike, bali mti wowote mkubwa ambao unatoa kivuli ulikuwa unatumika kama saluni au ofisi za kunyoa.

Chini ya mti utakuta viti kadhaa vya mbao na meza ambazo inakuwa imeegemezwa katikati ya mti. Kioo kikubwa nacho kinakuwa imefungwa kwenye mti na kuning'inia.

Watoto wa miaka ya 1970, 1980 na hata 1990, watakumbuka walivyokuwa wakipelekwa kwenye saluni hizo za kienyeji, ingawa wakati huo tulikuwa hatuiti saluni bali kwa kinyozi.

Wakifika hapo wanavingirishwa nguo nyeupe na kuwekwa kwenye kiti tayari kwa kunyolewa na mkasi, wakati mwingine ikichanganyika na wembe.

Tatizo kwenye baadhi ya miti hasa miembe kulikuwa na wadudu aina ya washawasha ambao walikuwa wanaleta usumbufu mkubwa.

Na mara nyingi watoto walipelekwa siku chache kabla ya sikukuu au kabla ya kufungua shule. Vinginevyo, baba mwenyewe, mama anaweza akamalizika na wewe nyumbani.

Twende kwa upande wa akinadada nao pia hawakuwa na saluni pia. Wao walikuwa wanasukana wenyewe kwa wenyewe. Mama mmoja alikuwa anaweza kutoka nyumbani kwake na kwenda kwa jirani na kuomba asukwe. Kama nafasi ipo wakati huo atasukwa, lakini kama hakuna atapewa ahadi baadaye, kesho au siku nyingine.

Wanawake walikuwa wakisukana bure kabisa. Labda ni kwa sababu wakati huo bado Watanzania walikuwa wanaishi kijamaa. Sikuwahi kuona hata siku moja mwanamke akimsuka mwenzake akalipwa kama ilivyo hivi sasa.

Wakati wa kusukana sasa, mmoja atakaa chini, iwe chini kabisa au kwenye mkeka. Msukaji atakaa kwenye kiti na chanuo. Hiki ndicho kinatumika kufumua nywele au kuzichana kabla ya kusukwa. Wanawake wakati huo walitumia kuanzia dakika 30 mpaka saa mbili kutengemea na aina ya nywele zinazosukwa.

Mitindo iliyotikisa sana wakati huo miaka ya 1970, 1980 hadi mwanzoni mwa 1990 ni ‘vitunguu’, ‘twende kilioni’, ‘uti wa roda’, ‘jicho la mke mwenza’, ‘mabutu’, ‘kilimanjaro’ na mingine mingi.

Hii ilikuwa kabla ya saluni kuenea kutokana na mabadiliko ya teknolojia, hasa baada ya umeme kusambaa.

Kabla ya hapo, tayari baadhi ya wanawake ambao walianza kujipambanua kuwa ni wa kisasa wakati ule, walikuwa wameshaanza kwenda mbali sana na kuchoma nywele zao.

Walikuwa wanatumia vitana vya chuma kuweka kwenye moto na baadaye kuzipitisha kwenye nywele.

Mtindo huu ulianza kuwa maarufu sana katikati ya miaka 1990 hadi mwanzoni mwa miaka ya 2000, ambapo teknolojia iliendelea kukua mno, badala ya kuzichoma, sasa zilikuwa zinawekwa kwenye mashine.

Wanawake waliochoma nywele na kupaka dawa za kuzifanya nywele kuwa nyeusi zaidi maarufu kama zazuu, walionekana warembo mno kutokana na kwamba ilikuwa haijazoeleka kuwaona wasichana au wanawake wakiwa kwenye mwonekano huo.

# HADITHI

KWANI mapenzi ni nini? Si kumpenda yule unayemtaka wewe? Kwa nini inafika wakati watu wanapangiana? Je, ukilazimisha yanaitwa mapenzi? Si yatafanana na utumwa? Yeyote anayetaka kulifanya penzi liwe na matabaka, rangi, kabila, anaweza kusababisha maafa makubwa. Donald. Kijana msomi aliyetoka Marekani, anarejea Tanzania. Akakabidhiwa kuendesha kampuni za baba yake lakini pia anatakiwa aoe. Hapo ndipo tatizo linapoanza. Usikose hata nakala moja ya riwaya hii tamu na ya kusisimua.

# Sumu ya Mapenzi-3

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

ILIKUWA wiki moja baada ya Donald kukutana na msichana Doris ambaye ameandaliwa kuwa mkewe. Shangazi na mama yake walimleta kwenye kasri lao. Waliwapa nafasi ya kukaa peke yao ili wapate muda wa kufahamiana.

Doris alikuwa msichana wa kisasa. Msomi na mwenye kila sifa ya kuitwa msichana mrembo. Alijipambanua kwa vipodozi vya gharama, nguo ghali na manukato ya thamani. Alikuwa zaidi ya hata baadhi ya wanawake ambao aliwaona nchini Marekani.

Donald alifurahi kuonana na Doris. Waliulizana maswali ya hapa na pale, pamoja na jinsi walivyokutanishwa na kwa lengo ya kutaka kuoana. Walizungumza mengi. Walikubaliana mengi na kila mmoja alibaki akiwa na furaha tele kwa kile kilichotokea kwa muda wa saa mbili waliokutana.

Kutokana na furaha kumzidi, Donald alimkumbuka rafiki yake mmoja aitwaye Sadiki. Huyu alikuwa rafiki yake mkubwa wakiwa kidato cha nne. Kila wanapotembea wapo wote. Wakifanya kosa, basi watafanya wote. Mmoja akipigana mwingine ataingilia. Walikuwa kama mapacha. Hata mmoja akimpata msichana, basi aliyebaki naye atamkata shoga ya msichana wa rafiki yake. Walishea furaha. Walishea na matatizo waliyoyapata. Kila mmoja alikuwa lazima amwambie mwenzake chochote kile ili awe na amani.

Tangu arejee nchini hakuwa na rafiki yeyote au mtu yeyote ambaye angeweza kukaa na kupiga naye stori. Kwanza ni kwa sababu malezi, kwani amelelewa kwenye familia ya kitajiri, ingawa hali hiyo aliiondoa kidogo alipokuwa shule na chuo ambako mara kwa mara alijaribu kujichanganya na watoto wa uswazi.

Kitendo cha kukutana na Doris, alionekana kumkumbuka Sadiki ili tu amwambie jinsi alivyompata msichana mrembo anayetarajiwa kuwa mkewe.

Akakumbuka mwezi mmoja uliopita alikutana na aliyekuwa mwanafunzi mwenzake mmoja na kumpa namba za simu za wanafunzi wengine mbalimbali na kumweleza wako wapi kwa sasa na wanafanya nini.




**Kitendo cha kukutana na Doris, alionekana kumkumbuka Sadiki ili tu amwambie jinsi alivyompata msichana mrembo anayetarajiwa kuwa mkewe. Akakumbuka mwezi mmoja uliopita alikutana na aliyekuwa mwanafunzi mwenzake mmoja na kumpa namba za simu za wanafunzi wengine mbalimbali na kumweleza wako wapi kwa sasa na wanafanya nini.**

Hata wale waliofariki dunia pia aliambiwa. Ya sadiki ilikuwa ya kwanza, kwani ndiye rafiki yake mkubwa. Akapiga. Haikupokewa kwa muda mrefu. Lakini wakati anataka kukata tamaa alisikia sauti "Halloo".

"Hallo, naongea na Sadiki?"

"Ndiyo mimi."

"Okay, mimi naitwa Donald."

"Donald, Donald yupi?"

"Yule unayemjua wewe."

"He wewe ni Donald kweli? Upo hapa nchini?"

"Ndiyo ndugu yangu, nipo hapa nina mwezi na nusu sasa."

Baada ya maongezi marefu kidogo, waliahidiana kukutana kesho yake.

Awali Donald alitaka kumkaribisha Sadiki nyumbani kwao Msasani Beach Mikoroshini.

Baada ya majadiliano yao ilionekana ni Donald inabidi aende mitaa ya Magomeni Makuti ili atakase macho, kwani tangu atoke Marekani ameendelea kung'ang'ania kukaa sehemu za kishua tu.

*************************

Gari aina ya Toyota Crown Athlete S210 rangi nyeusi lilionekana likitembea taratibu kwenye mitaa ya Magomeni Makuti.

Dereva aliyekuwa akiendesha gari hiyo alionekana akiongea na simu. Lakini mbele yake alikutana na kundi kubwa la watu likiziba hata barabara hiyo ya mitaani magari kupita.

Alisimamisha gari lake. Kundi la watu lingine lilionekana kushangilia na lingine kushangaa. Baada ya dakika mbili bila kuwa na dalili za kupita hapo, huku mwenyeji wake akimwambia ni lazima apite hapo ndipo afike nyumbani kwake, aliteremka. Nia ni kuangalia kuna nini na kama kuna namna yoyote ya kutatua tatizo.

Hakuzoea hali hiyo, lakini ilimbidi aingie kwenye kundi kubwa la watu ili aangalie mbele kuna nini.

Mbele aliona akinadada wawili wakipigana. Wapigana makonde, vibao na kuangushana chini. Alichoshangaa ni kwamba badala ya watu kuamulia, walikuwa wakiangalia kama pambano la masumbwi ambalo liko ulingoni na watu wamelipia kiingilio.

Tena wako waliokuwa wanashangilikia kabisa "Apigwe huyo kazoea."

Sekunde chache alizoangalia, ni kwamba mmoja alionekana kuzidiwa. Na hata pumzi zilimuishia. Hakusubiri.

Alijitosa katikati na kwenda kuamulia. Alimshika yule aliyeonekana kupigwa zaidi. Alionekana kutweta sana.

"Bahati yako wewe, ningekung'oa meno leo. Kwanza unajifanya unaringa sana. Ndiyo maana hata mtaani hupendwi mwanakharamu wewe. Nimeshakupiga na pesa zangu utanilipa, kunguni wewe."

Maneno hayo yalitoka kinywani kwa msichana mwingine ambaye yeye hakuwa ameshikwa.

Donald ndiye aliyeingilia ugomvi huo na kuuamua baada ya kuona hakuna juhudi zozote za umati wa watu wa uswahilini hapo kufanya hivyo.

"Kwani kuna tatizo gani?" Donald alimgeuka dada aliyekuwa hajamshika.

"Namdai pesa zangu shilingi laki mbili. Mimi nakopesha vitu kaka. Nguo za wanawake, watoto, vipodozi. Sasa nimemkopesha huyo bibie hadi zimefika laki mbili. Kulipa hataki ananipiga chenga. Ukienda kwake mara kajificha ndani, anawaambia ndugu zake kuwa na shoga zake kuwa hayupo, kumbe kajifungua. Mwezi sasa umepita. Leo nimemfuma hapa njiani. Ndiyo nimemfungia kazi."

"Eti ni kweli?" Dinald alimgeuka msichana aliyemwokoa kwenye kipigo na hadi wakati huo bado alikuwa amemshika kwa ajili ya ulinzi, ili aliyekuwa akipigana naye asifanye hivyo tena.

Hakujibu kitu. Aliendelea kutweta. Mwishoni alingua kilio. Hakikuwa cha sauti. Machozi yalionekana kumtiririka. Ilionekana ni hasira iliyochanganyikana na aibu.

Donald alimvuta msichana huyo akiwa bado ameshika. "Nifuate huku."

Alimwambia. "Na wewe pia njoo." Alimwita mwenzake.

Umati aliokuwa hapo ulikuwa haielewi nini kimetokea. Burudani yao ya ndondi imekatishwa ghafla na mtu ambaye hawamuelewi vema. Wengine walidhani kuwa labda ni askari.

Alifungua mlango wa gari na kuingiza mkono, kwenye droo, akatoa kibunda cha pesa na kuhesabu.

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# LULU DIVA AGUNAGUNA KUJICHUBUA

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Lulu Diva, ameibuka na kudai tuhuma anazopewa kwamba anatumia mkorogo ili awe mweupe haziwezi kumnyima usingizi.

Wiki hii msanii huyo amekabiliwa na maneno makali mtandaoni kutoka kwa mashabiki wake ambao wanasema mwonekano wake wa sasa ni dhahiri anatumia mkorogo na kujichubua.

Suala la mwonekano wangu ni wangu binafsi, hata nikitaka kuwa mwembamba nitakuwa nimeamua mwenyewe kwa sababu hata shabiki ana mwili wake, kama wanahisi hivyo, sawa siwezi kukaa kujieleza kama natumia losheni au la,' amesema Lulu Diva.

## Angella amlilia Ibiza Boy

KUFUATIA kifo cha mburudishaji wa kipindi cha Friday Night Live, David Urassa, wasanii mbalimbali wamejitokeza kumlilia na kusema ya moyoni.

Mwanamuziki wa kike kutoka Konde Gang, Anjella, amesema alifahamiana na'Ibiza Boy' kama mtoto wa mwenye nyumba yake wakati alipopanga na rafiki yake.

"Kwa niaba ya Konde Music Wordwide tunatoa pole kwa EATV nzima kwa kuondokewa na mfanyakazi mwenzao, namfahamu Ibiza Boy kama mtoto wa mwenye nyumba yangu sehemu ambayo nilikuwa naishi na rafiki yangu"

Amesema Anjella.

Ibiza Boy alifariki dunia siku ya Aprili 18, kwa ajali ya gari, na siku ya Aprili 23 amezikwa katika makaburi ya Kisota Kigamboni.



## Harmonize anavyoonyesha kiburi chake

JUZI mkali wa muziki wa Bongo Fleva, Harmonize, ametambulisha kibao chake kipya 'Altitude' akiwashirikisha mkongwe Awilo Longomba na H Baba.

Katika siku chache pekee, ngoma hiyo imeonekana kufanya vizuri na kusababisha wapenzi wa muziki nchini kuanza kuhoji nafasi ya mwanamuziki huyo kati ya washindani wake Diamond Platnumz na Ali Kiba.

Baadhi ya mashabiki wanasema wimbo huo unaonyesha jinsi Harmonize alivyokuwa na kiu ya kuwa kinara katika muziki nchini Tanzania na Afrika Mashariki na kati.



# Solkjaer amtaka Pjanic kutua Man United

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, ameishauri timu yake kumsajili, Miralem Pjanic ili awe mrithi wa kiungo, Paul Pogba ambaye anatajwa anataka kuondoka mwishoni mwa msimu huu.

Solskjaer amebainisha hayo baada ya tathmini ya muda kuhusu eneo lake la kiungo ambalo bado halijajua hatima ya Pogba klabuni hapo, ambaye amebakiza mkataba wa mwaka mmoja kuitumikia klabu hiyo.

Kwa upande wa Pjanic, toka ujio wa Kocha, Donald Koeman kule Barcelona amekuwa akipata wakati mgumu wa nafasi ya kucheza.

Kuna uwezekano mkubwa sasa anaweza kuondoka klabuni hapo majira yanayokuja ya kipindi cha joto.

Kwa BT Sport, Solskjaer anaamini kuwa Pjanic anaweza kuja kucheza pamoja na Scott McTominay na kufanya makubwa kabisa katika kikosi cha Manchester United.

Ikumbukwe kuwa ripoti hii imetolewa endapo tu Pogba ataondoka United.

Pogba ameeleza kwamba yupo katika kipindi cha furaha sana katika kikosi cha United na hakuna taarifa sahihi kama atasalia hapo au atatimka kwenda timu nyingine.

Klabu za Juventus ambako alicheza huko mwanzo kabla ya kurudi United na Real Madrid zimekuwa zikitajwa kuwania saini ya kiungo huyo.






# KOVACIC KUIKOSA REAL NUSU FAINALI

**LONDON,** England

KIUNGO wa Chelsea, Mateo Kovacic, anatarajiwa kukosa mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya timu yake ya zamani, Real Madrid pale kwenye dimba la Santiago Bernabeu.

Kocha, Thomas Tuchel, amethibitisha hayo kwenye mkutano wake na waandishi wa habari kabla ya mechi dhidi ya West ham iliyotarajiwa kuchezwa jana Jumamosi kwenye dimba la London.

Tuchel amethibitisha kikosi chote kipo tayari kwa ajili ya mchezo huo isipokuwa Kovacic, ambaye amekuwa akiendelea vizuri, lakini hatakuwa na haraka ya kushiriki katika mojawapo ya mechi mbili zijazo.

"Mateo Kovacic bado yuko nje, lakini kuna mtu mwingine atapatikana," alisema Tuchel akiwaambia waandishi wa habari.

"Kwa mimi binafsi, nadhani tunaweza kumtumia, lakini lazima tuchukue ushauri wa matibabu.

"Labda madaktari watazuia kwa hilo, lakini nadhani inawezekana akarudi tena dhidi ya Fulham, mchezo ambao upo kati ya michezo ya Madrid," aliongeza.

# *Kane hatihati kucheza fainali*

**LONDON,** England

NAHODHA wa Tottenham Hotspur, Harry Kane, ana hatihati ya kukosekana katika mchezo wa fainali ya Kombe la EFL (Carabao) dhidi ya Manchester City utakaochezwa leo Jumapili.

Kane aliumia kifundo cha mguu Ijumaa iliyopita wakati timu yake ilipokuwa ikichuana dhidi ya Everton katika mchezo ambao ulikuwa ni wa mwisho kwa Kocha, Jose Mourinho kabla ya kufukuzwa kwenye timu hiyo.


Nyota huyo mwenye umri wa miaka 27, alikosa mchezo kati ya timu yake ya Tottenham dhidi ya Southampton ambapo ilishinda mabao 2-1 kwenye Ligi Kuu England kutokana na maumivu ya goti.

Taarifa zimeeleza kuwa Kane ambaye ni namba moja kwa utupiaji katika kikosi hicho akiwa amefunga jumla ya mabao 26 katika mashindano yote, alianza mazoezi na wenzake lakini hali ya kuwa fiti kwa ajili ya mchezo wa leo bado haijajulikana.

Mchezo huo unatarajiwa kuchezwa kwenye dimba la Wembley.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# CAVANI ATANGAZA KUONDOKA UNITED

## Awasilisha rasmi maombi kwa mabosi wake na kusema amefikia uamuzi huo kwa sababu...

**MANCHESTER,** England

MSHAMBULIAJI Edinson Cavani amewasilisha rasmi maombi ya kutaka kuondoka Manchester United na kujiunga na Boca Juniors, kwa mujibu wa BT Sport.

**Cavani katika maombi hayo pia ameweka wazi anataka kuwa karibu na familia yake na hivyo anataka kuondoka mara mkataba wake utakapomalizika mwishoni mwa msimu huu.**

Kwa mujibu wa ripoti, Cavani alikutana na maofisa wa United na kuzungumza nao kuhusu mpango wake huo juzi Ijumaa.

Cavani ataondoka United ambako amecheza kwa kipindi cha msimu mmoja na baba yake amebainisha kuwa ameshawasiliana na Boca Juniors ya nchini Argentina kwa ajili ya kujiunga nao katika kipindi cha majira ya joto kinachokuja.

Cavani alitua pale Old Trafford kwa uhamisho wa bure kutoka PSG mwanzoni mwa msimu huu, ambako alisaini mkataba wa mwaka mmoja na kipengele cha kuongezewa miezi 12 mingine.

Mshambuliaji huyo mkongwe amefunga mabao matatu katika michezo yake mitatu iliyopita na klabu hiyo ina hamu ya kuongeza mkataba wake hadi msimu ujao.

Lakini mchezaji mwenyewe ambaye ana umri wa miaka 34 ameweka wazi nia yake ya kutaka kuondoka baada ya kufanya mazungumzo na maofisa wa United.

Cavani aliiambia klabu hiyo anataka kurudi Amerika Kusini ili kuwa karibu na familia yake, na ripoti hiyo inaongeza kuwa alizikataa timu kadhaa za Brazil zilizokuwa zinawania saini yake ili tu ajiunge na Boca juniors.

## ZISIKUPITE

### LIVERPOOL, KONATE SAFI

LIVERPOOL imefikia makubaliano binafsi na mlinzi wa RB Leipzig, Ibrahima Konate mwenye umri wa miaka 21, ambaye kipengele cha mkataba wake wa kuondoka kwa miamba hao wa Bundesliga ni pauni milioni 34. ***(Fabrizio Romano on Twitter)***

### MESSI KUPEWA MITATU

RAIS wa Barcelona, Joan Laporta, anafanyia kazi mchakato wa ofa ya mkataba wa miaka mitatu kwa straika wa Argentina, Lionel Messi, katika jaribio la kumshawishi mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 kubakia klabuni hapo. ***(ESPN)***

### RONALDO KUREJEA UNITED

MSHAMBULIAJI wa Juventus na Timu ya Taifa ya Ureno, Cristiano Ronaldo, mwenye umri wa miaka 36, anataka kurudi Manchester United katika kipindi cha majira ya joto. ***(Gazzetta dello Sport)***

### KING ANUKIA GALATASARAY

STRAIKA wa Everton, Josh King, yupo kwenye mazungumzo na klabu ya Uturuki ya Galatasaray na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 anataka kujiunga nayo kipindi cha majira ya joto. ***(Football Insider)***

### ODEGAARD AZUA HOFU

ARSENAL inahofia wanaweza kumpoteza kiungo wa kimataifa wa Norway, Martin Odegaard mwenye umri wa miaka 22, ambaye anacheza kwa mkopo kutoka Real Madrid. ***(Sun)***

### BERGE HAONDOKI

KOCHA wa muda wa Sheffield United, Paul Heckingbottom anatarajia kiungo wa Norway, Sander Berge (23), atabakia klabuni hapo baada ya timu hiyo kushuka daraja, licha ya kutolewa macho na Arsenal na Tottenham Hotspur. ***(Sheffield Star)***

### RUIZ-ATIL KUREJEA BARCA

BARCELONA inajaribu kumrudisha kiungo wa Ufaransa, Kays Ruiz-Atil (18), klabuni hapo, huku mkataba wake ukitarajiwa kumalizika kule Paris St-Germain mwishoni mwa msimu huu. ***(Mundo Deportivo)***

### GRANT NJIA MOJA

GOLIKIPA namba tatu wa Manchester United, Lee Grant mwenye umri wa miaka 38, anatarajia kuondoka klabuni hapo katika kipindi cha majira ya joto. ***(Mail)***

### POTTER KUIMARIKA

KOCHA wa Brighton, Graham Potter amesema kiungo wa Mali, Yves Bissouma anaweza kuimarika klabuni hapo na hivyo hawatakiwi kuwa na hofu kuhusu nyota huyo mwenye umri wa miaka 24. ***(Express)***

### WOODWARD KURITHIWA

MAKAMU Mwenyekiti Mtendaji wa Manchester United, Ed Woodward, anayeondoka klabuni hapo anatarajia kuchagua mrithi wake hivi karibuni. ***(Manchester Evening News)***

# Ihefu SC, Coastal Union hapatoshi

**Na Mwandishi Wetu,** MBARALI

KOCHA Mkuu wa Ihefu SC, Zuberi Katwila, amesema kikosi chake kitaendelea kupambana kuhakikisha kinapata ushindi katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Coastal Union itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Highland Estates ulioko mjini hapa.

Ihefu itashuka dimbani leo ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa bao 1-0 dhidi ya 'Maafande' wa Tanzania Prisons walioupata Alhamisi iliyopita kwenye uwanja huo.

Katwila (pichani) aliliambia gazeti hili anahitaji kupata ushindi kwa ajili ya kuendelea kufufua matumaini ya kubakia katika ligi hiyo na anaamini nafasi ya kutimiza ndoto zao bado wanayo.

Kocha huyo alisema mechi zote wanazocheza ni ngumu na zenye ushindani, lakini amewaandaa wachezaji wake kutokata tamaa kwa sababu kila timu inaingia uwanjani kwenye hatua hii ya lala salama ikiwa na malengo yake.

"Tutapambana hadi siku ya mwisho, hatutabweteka, hatutaki kuangalia tulipokosea nyuma, tunajipanga kusaka matokeo mazuri katika mechi zilizobakia, tunaamini nafasi ya kubakia bado ipo kama mambo yatakwenda vizuri," alisema Katwila.



Golikipa namba moja wa timu hiyo, Deogratius Munisi 'Dida' alisema mechi zote wanazocheza ni ngumu na hii inasababishwa na ushindani ulioongezeka msimu huu.

Dida alisema ataendelea kujipanga imara kuhakikisha anaibakisha timu hiyo kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kumsajili ili kuongeza nguvu katika kikosi hicho.

Naye Kocha Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda alisema wamekwenda Mbeya kwa ajili ya kusaka matokeo mazuri kwa sababu kikosi chake bado hakiko katika nafasi salama kwenye msimamo wa ligi.

"Hatuko katika nafasi nzuri au salama, tunahitaji kupata ushindi ili kuendelea kujiimarisha, hakuna mechi rahisi, tumejiandaa kupambana," Mgunda alisema.

Ihefu SC yenye pointi 27 baada ya kucheza mechi 27 imebakiza mechezo saba ili kumaliza msimu wake wa kwanza ndani ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

# UHURU AFUNGUKA SIMBA INAVYOMVURUGA LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

WINGA wa Mwadui FC ya Shinyanga, Uhuru Selemani, amesema anapata wakati mgumu kila anapocheza dhidi ya timu yake ya zamani ya Simba katika mechi mbalimbali za Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano mengine yanayofanyika hapa nchini, imefahamika.

**Akizungumza na gazeti hili Uhuru alisema anakuwa kwenye hali yenye 'mawazo' anapokutana na Simba kwa sababu ndiyo timu pekee ambayo ameichezea kwa miaka mwingi hapa nchini.**

"Inaumiza kwa kweli kucheza dhidi ya Simba. Hii timu nimecheza miaka sita na ndiyo timu niliyokaa nayo muda mrefu sana kuliko timu yoyote ile, kwa hiyo kucheza dhidi yake inaniumiza moyoni," alisema Uhuru.

Winga huyo ambaye aliuzwa kwenye klabu ya Royal Eagles ya Afrika Kusini, alicheza vyema katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya mabingwa hao watetezi iliyochezwa Jumapili iliyopita aliwadhibiti vyema wachezaji wa Simba katika mchezo uliomalizika kwa Wekundu wa Msimbazi kushinda bao 1-0.

"Ni kweli nilicheza vizuri kwa sababu ile ni kazi yangu, ni lazima nifanye kazi kwa ajili ya timu yangu ya sasa na hiyo na ndiyo uanamichezo, lakini haiondoi ukweli kuwa kila nilipokuwa naiangalia jezi ya Simba, nilikuwa najiuliza ni kwa nini nacheza dhidi ya timu hii, kwa sababu hata nikirudi nyumbani nikifungua kabati, unakutana na jezi za Simba ambazo nimezitumikia kwa miaka sita. Lakini yote ni maisha, huwezi kujua nini ninatokea," Uhuru alisema.

Kuhusu matokeo ya kusuasua kwa Mwadui, winga huyo alisema hali hiyo inatokana na hali mbaya ya kiuchumi iliyopo kwenye klabu hiyo.

"Asikudangaye mtu, mpira ni pesa. Timu iko kwenye hali mbaya kiuchumi. Maisha yanapokuwa mabovu hata kujiamini kunapotea. Hata tunavyocheza unaona kwa mchezaji mmoja mmoja sisi ni wazuri kwa sababu baadhi yetu ni wachezaji wakubwa, lakini kila mtu anacheza kivyake kwa sababu uchumi wa klabu si mzuri," aliongeza nyota huyo.

Uhuru, ambaye aliichezea Simba kuanzia mwaka 2009, hadi 2015, alisema inamuuma mno kucheza dhidi ya timu yake ya zamani, lakini haina jinsi kwa sababu mpira ni kazi yake na anaamini amecheza kwa nguvu zote kuizuia timu hiyo isishinde, lakini ikashindikana.

Mbali ya Uhuru, Mwadui ilichezesha wachezaji wengi wa zamani wa Simba akiwamo Aziz Gilla na Willian Lucian 'Gallas'. Mwadui inatarajiwa kuendelea kusaka pointi za kujinasua na janga ya kushuka daraja kwa kuwafuata wenyeji wao Ruvu Shooting kwenye Uwanja wa Mabatini, Mlandizi mkoani Pwani.



Kiungo wa kimataifa wa Simba Queens Mkongomani, Mawete Musolo (kulia), akijiandaa kumtoka beki wa Alliance Girls katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania iliyochezwa kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza juzi. Simba Queens ilishinda mabao 5-0. **PICHA: SIMBA**

# Makundi ufukweni Afrika hadharani

**Na Saada Akida**

SHIRIKISHO la Soka Afrika (CAF), linatarajia kuchezesha droo ya makundi kwa ajili ya Fainali za Mataifa ya Afrika kwa soka la ufukweni (Afcon- Beach Soccer), ambazo zitachezwa kuanzia Mei 23 hadi 29, mwaka huu nchini Senegal.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kocha Mkuu wa timu ya Tanzania, Boniface Pawassa alisema kikosi chake kinaendelea vizuri na maandalizi ya michuano hiyo na wako tayari kukutana na kikosi chochote.

Pawasa alisema wachezaji wake wanaendelea kuimarika baada ya kufanya mazoezi mfululululizo kwa muda wa wiki mbili sasa.

"Tunaendelea na maandalizi na sasa ni wiki ya pili ya mazoezi ya kiufundi, mbinu, ujanja na ubunifu na wiki ya tatu tutakuwa na mechi za kirafiki, tukitarajiwa kucheza mechi za kirafiki na wenyeji wa michuano hiyo ambao ni Senegal," alisema Pawassa.

Kocha huyo aliongeza mbali na Senegal kuomba mechi ya kirafiki dhidi yao, pia wameomba kukutana na Cape Verde, Morocco na Dubai ili kuendelea kujiimarisha zaidi.

"Malengo yetu makubwa katika fainali hizo ni kufanya vizuri na kuwa miongoni mwa timu kutoka bara la Afrika zitakazokwenda kushiriki Kombe la Dunia la huko Urusi Septemba mwaka huu," alisema Pawassa.

Tanzania ilifuzu kucheza fainali hizo baada ya kuwaondoa Burundi kwa jumla ya mabao 12-9, mechi zote mbili zikichezwa kwenye Ufukwe wa Coco, uliopo jijini Dar es Salaam.

Michezo
Jumapili Aprili 25, 2021
Nipashe




Cavani atangaza kuondoka United

UKURASA 22




Mshambuliaji wa Simba, John Bocco (kulia), akikokota mpira huku kiungo mkabaji wa Gwambina FC, Baraka Mtui, akimdhibiti katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Gwambina ulioko Misungwi jijini Mwanza. Simba ilishinda bao 1-0. **PICHA: SIMBA**

## Yanga, Azam heshima, kisasi

**Na Saada Akida**

NI mechi ya kisasi, unaweza kusema hivyo baada ya makocha wa timu zote mbili, Yanga na Azam FC kusema kila mmoja anahitaji pointi tatu muhimu katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayowakutanisha leo usiku kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Yanga ambao ni wenyeji wa mchezo huo wanahitaji kupata matokeo chanya ili kujiimarisha katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara sambamba na Azam, lakini pia zikijiweka katika nafasi nzuri ya kupata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya msimu ujao.

Azam itateremka katika mchezo huo ikiwa na kumbukumbu ya kuchapwa bao 1-0 na wapinzani wao katika mchezo wa mzunguko uliochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini.

Kocha wa Makipa wa Yanga, Razak Siwa, alisema kikosi chao kipo fiti na hawataingia kwa tahadhari yoyote katika mchezo huo lakini wanahitaji kusaka pointi tatu.

"Ni mechi ya ushindani ukizingatia wapinzani wetu Azam FC, wanahitaji kulipa kisasi kutokana na mechi ya kwanza kupoteza, na kutohitaji kupoteza tena, sisi pia tunahitaji kupata pointi muhimu ili kujiimarisha vizuri katika nafasi tuliyopo kwenye msimamo," alisema Siwa.

Kocha huyo alisema wachezaji wote wako fiti isipokuwa Tuisila Kisinda ambaye afya yake haiko sawa na nafasi ya kuonekana katika mechi hiyo iko kwenye hatihati.

Nahodha wa Yanga, Ramadhani Kabwili alisema makocha wamemaliza majukumu yao na kilichobakia ni kwa upande wa wachezaji kupambana na kupata matokeo chanya ya pointi tatu.

Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, alisema hawana majeruhi na wamejipanga vizuri kuhakikisha hawapotezi mechi hiyo ya marudiano na hivyo watacheza kwa tahadhari kubwa ya kupata ushindi.

Naye nahodha wa Azam FC, Aggrey Morris, alisema wamejipanga vizuri na kuhakikisha wanalipa kisasi baada ya kupoteza mechi mbili dhidi ya Yanga, moja katika ligi na nyingine kwenye michuano ya mapinduzi ndani ya msimu huu.

# Simba yapaa kileleni Bara

### ●●● Ni baada ya kuichapa Gwambina bao 1-0 na kujiimarisha katika...

**Na Adam Fungamwango**

KWA mara ya kwanza mabingwa watetezi, Simba, wamekwea kileleni katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Gwambina FC katika mechi ya ligi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Gwambina FC, Misungwi jijini Mwanza.

**Lilikuwa ni bao la beki wa kushoto, Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr, lililowafanya mabingwa hao watetezi, Simba, kuongoza ligi baada ya kufikisha pointi 58, pointi moja nyuma ya Yanga iliyokuwa inaongoza kwa muda mrefu.**

Hata hivyo, Simba kuendelea kuongoza ligi kunategemea matokeo ya mechi ya leo usiku kati ya wenyeji Yanga dhidi ya Azam.

Kama Yanga itafungwa au kutoa sare yoyote basi Simba itaendelea kuwa kileleni, lakini ushindi wowote wa Wanajangwani hao utawafanya kwenda tena juu ya msimamo kwa pointi 60.

Dakika ya saba tu ya mchezo faulo iliyopigwa kulia mwa goli la Simba na Baraka Mtui, lilileta kizaazaa na wachezaji Gwambina kushindwa kuuweka mpira wavuni, mpaka mabeki wa timu hiyo inayoshiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika wakaokoa. Nahodha, John Bocco, ilikuwa aipatie timu yake bao dakika ya 22, baada ya kumegewa pande safi kutoka kwa Meddie Kagere lakini shuti lake dhaifu liliishia mikononi mwa golikipa wa Gwambina, Mohamed Makaka.

'Zimbwe Jr', alifunga bao pekee kwenye mechi hiyo dakika ya 28 alipoupata mpira uliookolewa kizembe na mabeki wa Gwambina, akiwa umbali wa mita 35 aliachia shuti kali la juu lililogonga pembezoni mwa mwamba wa juu na kudundadunda wavuni, Makaka akiruka bila mafanikio.

Hata hivyo, muda mrefu wa mechi hiyo, timu zote zilikuwa zikicheza mipira mirefu na kukimbizana badala ya kupigiana pasi kutokana na hali mbaya ya uwanja huo.

Gustapha Simon ambaye alikuwa kwenye kiwango cha juu kwenye mechi hiyo, alipata nafasi nzuri ya kuisawazishia Gwambina FC bao dakika ya 45, akiwa anatazamana na kipa wa Simba, Aishi Manula, lakini alipiga shuti kali lililotoka nje kidogo ya lango.

Kipindi cha pili timu zote ziliendelea kucheza kwa mfumo ule ule, ambao ulionekana kuinufaisha zaidi Gwambina kuliko Simba lakini Wekundu wa Msimbazi walianza kubadilika mara alipotoka Bernard Morrison na kuingia Hassan Dilunga na Chris Mugalu ambao waliituliza timu yao na kuanza kupiga pasi.

Mechi iliingia dosari dakika ya 74, baada ya Joash Onyango kuweka mpira wavuni uliotokana mpira wa kona, lakini mwamuzi msaidizi namba moja, Geofrey Msakila, alilikataa kwa madai kuwa kabla ya kufungwa mpira huo ulitoka nje.

Kukataliwa kwa bao hilo kulizusha kizaazaa kwa mashabiki kuanzisha fujo kwa kurusha chupa uwanjani, na askari polisi ilibidi wafanye kazi ya ziada kutuliza rabsha hizo.

Katika mechi nyingine ya mapema iliyochezwa jana, Mbeya City imeendelea kuzinduka baada ya kuifunga Namungo FC bao 1-0 katika mchezo uliofanyika kwenye Uwanja wa Majaliwa mkoani Lindi.

Simba itashuka tena ugenini Jumanne kuwakabili Dodoma Jiji FC kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >